REPUBLIC OF KENYA

# MINISTRY OF EDUCATION

# UPPER PRIMARY LEVEL DESIGNS

## SUBJECT

# KISWAHILI

## GRADE 6

KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT

JANUARY 2021

First Published in 2021

All rights reserved. No part of this book may be reproduced, stored in a retrieval system or transcribed in any form or by any means; electronic, mechanical, photocopy, recording or otherwise, without the prior written permission of the publisher.

**ISBN:**

Published and printed by Kenya Institute of Curriculum Development

## FOREWORD

The Government of Kenya is committed to ensuring that policy objectives for education, training and research meet the aspirations of the Kenya Constitution 2010, the Kenya Vision 2030, the United Nations Sustainable Development Goals (SDGs) and the Regional and Global conventions to which Kenya is a signatory. In relation to this, the Ministry of Education (MoE) embarked on curriculum reforms that culminated in the full implementation of the Competency Based Curriculum (CBC) in January, 2019 from the level of Early Years Education (Pre-Primary 1 and 2, and Lower Primary Grade 1, 2 and 3). This was followed by the roll out of the curriculum in Grade 4 in 2020. In readiness for the progression of the Grade 4 cohort, the curriculum designs for Grade 5 were developed.

Grade 6 designs have now been developed. These curriculum designs are intended to ensure that the core competencies attained by learners at Grade 5 are enhanced even as further opportunities are provided for identification and nurturing of every learner's potential as learners prepare to transit to Junior Secondary school.

The curriculum designs include the general and specific learning outcomes for the learning areas (subjects) as well as strands and sub - strands. The designs also outline suggested learning experiences, key inquiry questions, assessment rubric, pertinent and contemporary issues, values and Community Service Learning (CSL) activities.

It is my hope that all Government agencies and other stakeholders in Education will use the designs to plan for effective and efficient implementation of the Competency Based Curriculum.

**PROF. GEORGE A. O. MAGOHA, MBS, EBS, CBS**

**CABINET SECRETARY**

**MINISTRY OF EDUCATION**



Not for Sale

## PREFACE

The Ministry of Education (MoE) is currently implementing the second phase of the curriculum reforms with the roll out of the Competency Based Curriculum (CBC) at Grade 4 in 2020. This is the first cohort of the Upper Primary level in the new education structure. Grade 5 and 6 designs have also been developed.

Grade 6 being the final stage of the upper primary level is very critical in the realization of the Vision and Mission of the on-going curriculum reforms as enshrined in the Sessional Paper No. I of 2019 whose title is: *Towards Realizing Quality, Relevant and Inclusive Education and Training for Sustainable Development* in Kenya. The Sessional Paper explains the shift from a Content - Focused Curriculum to a focus on **Nurturing every Learner's potential.**

Therefore, the Grade 6 curriculum designs are intended to enhance the learners' development in the CBC core competencies, namely: Communication and Collaboration, Critical Thinking and Problem Solving, Creativity and Imagination, Citizenship, Digital Literacy, Learning to Learn and Self-efficacy.

The curriculum designs also continue to link the activities in the main learning areas to the other aspects of the CBC including links to Pertinent and Contemporary Issues (PCIs), Values and Community Service Learning (CSL). The designs also offer several suggested interactive learning activities and variety of assessment techniques. It is expected that the curriculum designs will guide the teachers to enable learners attain the expected learning outcomes for Grade 6 and prepare them effectively for the next Grade.

It is my expectation that the teacher will use the designs to make learning interesting, exciting and enjoyable.

**DR. BELIO R. KIPSANG, CBS**
**PRINCIPAL SECRETARY**
**STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION**
**MINISTRY OF EDUCATION**

## ACKNOWLEDGEMENT

The Kenya Institute of Curriculum Development (KICD) Act Number 4 of 2013 (Revised 2018) mandates the Institute to develop curricula and curriculum support materials for basic and tertiary education and training, below the university. The curriculum development process for any level involves thorough research, international benchmarking and robust stakeholder engagement. Through this systematic and consultative process, the KICD conceptualised the Competency Based Curriculum (CBC) as captured in the Basic Education Curriculum Framework (BECF), that responds to the demands of the 21st Century and the aspirations captured in the Kenya Constitution 2010, Kenya and the Kenya Vision 2030, East African Commission Protocol and the United Nations Sustainable Development Goals.

KICD obtains its funding from the Government of Kenya to enable the successful achievement of the stipulated mandate and implantation of the Government and Sector (Ministry of Education (MoE) plans. The Institute also receives support from development partners targeting specific programmes. The Grade 6 curriculum designs have been developed with the support of the World Bank through the Kenya Secondary Education Quality Improvement Program (SEQIP) commissioned by the MoE. Therefore, the Institute is very grateful for the support of the Government of Kenya, through the MoE and the development partners for the policy, resource and logistical support. Specifically, special thanks to the Cabinet Secretary – MoE and the Principal Secretary – State Department of Early Learning and Basic Education,

We also wish to acknowledge the KICD curriculum developers and other staff, all teachers, educators who took part as panelists; the Semi-Autonomous Government Agencies (SAGAs) and representatives of various stakeholders for their various roles in the development of the Grade 6 curriculum designs. In relation to this, we acknowledge the support of the Secretary - Teachers Service Commission (TSC) and the Chief Executive Officer of the Kenya National Examinations Council (KNEC) for their support in the process of developing these designs.

Finally, we are very grateful to the KICD Council Chairperson Dr. Sara Ruto and other members of the Council for very consistent guidance in the process. We assure all teachers, parents and other stakeholders that these curriculum designs will effectively guide the implementation of the CBC at Grade 6 and preparation of learners for Grade 7.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO**
**DIRECTOR/CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT.**

**TABLE OF CONTENTS**

FOREWORD ........................................ iii

PREFACE ........................................ iv

ACKNOWLEDGEMENT ........................................v

TABLE OF CONTENTS ........................................ vii

NATIONAL GOALS OF EDUCATION ........................................ viii

SUGGESTED TIME ALLOCATION........................................x

GENERAL LEARNING OUTCOMES FOR MIDDLE SCHOOL ........................................ xi

KISWAHILI ........................................ 1



Not for Sale

## NATIONAL GOALS OF EDUCATION

### 1. Foster nationalism, patriotism, and promote national unity

Kenya's people belong to different communities, races and religions and should be able to live and interact as one people. Education should enable the learner acquire a sense of nationhood and patriotism. It should also promote peace and mutual respect for harmonious co-existence.

### 2. Promote social, economic, technological and industrial needs for national development

Education should prepare the learner to play an effective and productive role in the nation.

**a)** Social Needs Education should instil social and adaptive skills in the learner for effective participation in community and national development.

**b)** Economic Needs Education should prepare a learner with requisite competences that support a modern and independent growing economy. This should translate into high standards of living for every individual.

**c)** Technological and Industrial Needs Education should provide the learner with necessary competences for technological and industrial development in tandem with changing global trends.

### 3. Promote individual development and self-fulfilment

Education should provide opportunities for the learner to develop to the fullest potential. This includes development of one's interests, talents and character for positive contribution to the society.

### 4 Promote sound moral and religious values

Education should promote acquisition of national values as enshrined in the Constitution. It should be geared towards developing a self- disciplined and ethical citizen with sound moral and religious values.

**5. Promote social equity and responsibility**

Education should promote social equity and responsibility. It should provide inclusive and equitable access to quality and differentiated education; including learners with special educational needs and disabilities. Education should also provide the learner with opportunities for shared responsibility and accountability through service learning.

**6. Promote respect for and development of Kenya's rich and varied cultures**

Education should instil in the learner appreciation of Kenya's rich and diverse cultural heritage. The learner should value own and respect other people's culture as well as embrace positive cultural practices in a dynamic society.

**7. Promote international consciousness and foster positive attitudes towards other nations**

Kenya is part of the interdependent network of diverse peoples and nations. Education should therefore enable the learner to respect, appreciate and participate in the opportunities within the international community. Education should also facilitate the learner to operate within the international community with full

knowledge of the obligations, responsibilities, rights and benefits that this membership entails.

**8. Good health and environmental protection**

Education should inculcate in the learner the value of physical and psychological well-being for self and others. It should promote environmental preservation and conservation, including animal welfare for sustainable development.



Not for Sale

# SUGGESTED TIME ALLOCATION

| # | Subject | Lessons Per Week |
|---|---|---|
| | Mathematics | 5 |
| | Physical and Health Education | 5 |
| | English language | 4 |
| | Kiswahili Language KSL for learners who are deaf | 4 |
| | Science and Technology | 4 |
| | Agriculture | 3 |
| | Creative Arts (Art and craft, Music) | 3 |
| | Home science | 3 |
| | Religious Education (CRE/IRE/ HRE) | 3 |
| | Social Studies (Citizenship, Geography, History) | 3 |
| | Other Languages | 2 |
| | Pastoral Programme and Instructions | 1 |
| | **TOTAL** | **40** |

# GENERAL LEARNING OUTCOMES FOR MIDDLE SCHOOL EDUCATION

By the end of Middle School, the learner should be able to:

1) Apply Literacy, Numeracy Skills and Logical Thinking Appropriately in Self-Expression,
2) Communicate Effectively in Diverse Contexts,
3) Apply Digital Literacy Skills Appropriately for Communication and Learning in Day-To-Day Life,
4) Practise Hygiene, Appropriate Sanitation and Nutrition to Promote Health,
5) Explore, Manipulate, Manage and Conserve the Environment Effectively For Learning And Sustainable Development,
6) Demonstrate Ethical Behaviour and Exhibit Good Citizenship as A Civic Responsibility,
7) Demonstrate Social Skills, Spiritual and Moral Values for Peaceful Co-Existence,
8) Demonstrate Appreciation of The Country's Rich, Diverse Cultural Heritage for Harmonious Co-Existence,
9) Manage Pertinent and Contemporary Issues in Society Effectively.



Not for Sale

# KISWAHILI



Not for Sale

## KAULI KIINI

Mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika shule ya msingi daraja la juu atajenga stadi na umahiri ufaao kuwasiliana, kutangamana na kushiriki katika miktadha mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutumia lugha kuzungumza na kuandika. Mwanafunzi anahitaji kujifunza kunga za Kiswahili ili kuitumia lugha hii kama wenzo wa ujifunzaji. Aidha, mwanafunzi hufunzwa Kiswahili ili kushiriki na kukichangamkia katika hali zake mbalimbali. Hili humwezesha kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa kujifunza sarufi na matumizi ya Kiswahili kimuktadha, mwanafunzi anaweza kuwasiliana kwa ufasaha, umahiri na kwa namna ambayo itaimarisha utangamano darasani na katika ulimwengu mpana. Nadharia ya sarufi bia ya Noam Chomsky (1965), inaeleza kuwa binadamu ana uwezo asilia wa kuvimudu vipengele vya kisarufi. Uwezo huu huchangia katika ukuaji wa lugha wa mwanafunzi na hivyo kumfanya mzungumzaji stadi wa lugha anayeweza kubaini matumizi sahihi na yasiyo sahihi.

### Matokeo Tarajiwa ya Kijumla katika Somo la Kiswahili, Kiwango cha Shule ya Msingi Daraja la Juu

Kufikia mwisho wa shule ya msingi daraja la juu, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano
b) kuzingatia kanuni za lugha kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi
c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali
d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti
maishani
e) kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali
f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

| 1.0 VIUNGO VYA MWILI VYA NDANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli Za Ujifunzaji** | **Maswali Dadisi** |
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Matamshi Bora: Silabi na Vitanzandimi**<br><br>**Sauti: d/nd<br>ch/sh<br>j/nj<br>g/ng**<br><br>**(Vipindi 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno<br>b) kutamka silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuimarisha matamshi<br>c) kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuimarisha matamshi bora<br>d) kuunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa ili kukuza ubunifu<br>e) kuchangamkia kukariri | Mwanafunzi:<br>• atambue silabi za sauti, d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng (*k.v. doa/ndoa, choka/shoka, jaa/njaa, goma/ngoma*) kutokana na maneno kwenye vitabu, ubaoni au kwa kutumia vifaa vya kidigitali<br>• asikilize silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidigitali (*k.v. kinasasauti*)<br>• atamke silabi za sauti lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawiliwawili au katika kikundi<br>• asikilize vitanzandimi vinavyoundwa kutokana na maneno yenye sauti lengwa vikikaririwa (*k.v. Mkunjo ulikunjwa na waja wenye njaa kukicha*)<br>• aunde vitanzandimi vinavyotokana na vitate husika akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• awasilishe vitanzandimi alivyounda darasani ili wenzake wamtolee | 1. Je, unajua maneno gani yenye silabi za sauti d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng?<br>2. Je, Unajua vitanzandimi gani vyenye silabi za sauti d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuimarisha matamshi. | maoni<br>• ashiriki katika kutoa maoni kuhusu vitanzandimi vya wenzake kwa upendo na heshima<br>• aunde vitanzandimi kwenye vifaa vya kidijitali kwa kushirikiana na wenzake mitamboni na kuvirekebisha. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala kuhusu vitanzandimi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kidijitali vinapotumiwa kusikiliza sauti na kuunda vitanzandimi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapounda vitanzandimi vyenye maana kutokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi.
- Ubunifu – mwanafunzi anaposhiriki katika kuunda vitanzandimi vyenye maana.

**Uhusiano na masuala mtambuko:**

- Stadi za maisha – mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika vikundi na kujifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini.

**Uhusiano na Maadili:**

- Heshima na ushirikiano – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- English language na Indigenous Language – masomo haya yanashughulikia dhana ya silabi na vitanzandimi.

**Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**

- Kuwashirikisha wenzake katika jamii (ikiwemo jamii ya shule) kuhusu uimarishaji wa matamshi bora kupitia kukariri vitanzandimi.
- Kujifunza kutoka kwa wanajamii kuhusu vitanzandimi vinavyotumiwa na jamii hiyo.

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua ipasavyo silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno. | Anatambua ipasavyo na kwa urahisi silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno. | Anatambua ipasavyo silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno. | Anatambua ipasavyo baadhi ya silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno. | Anatatizika kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno. |
| Kutamka ipasavyo silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatamka ipasavyo na kwa wepesi silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatamka ipasavyo silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatamka ipasavyo baadhi ya silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Ana changamoto kutamka silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi. |
| Kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa usahihi. | Anatamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa usahihi na wepesi. | Anatamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa usahihi. | Anatamka baadhi ya vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa usahihi. | Anatamka baadhi ya vitanzandimi vinavyoundwa kwa baadhi ya silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi. |
| Kuunda vitanzandimi | Anaunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na | Anaunda vitanzandimi vyenye | Anaunda baadhi ya vitanzandimi vyenye | Anaunda baadhi ya vitanzandimi kutokana |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa. | silabi za sauti lengwa kwa ufasaha na urahisi. | maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha. | maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha. | na baadhi ya silabi za sauti lengwa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Kifungu cha Hadithi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu<br>b) kueleza maana ya msamiati lengwa ili kuubainisha<br>c) kusoma kifungu cha hadithi akizingatia ujumbe<br>d) kuonyesha ufahamu wa kifungu kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari<br>e) kuchangamkia usomaji ili kuimarisha ufahamu. | Mwanafunzi:<br>• atambue viungo vya mwili vya ndani (*k.v. moyo, mapafu, ini, kibofu, wengu, figo, ubongo, mifupa na mishipa*) kutokana na picha, chati au kwenye tarakilishi<br>• aeleze maana za msamiati alioutambua<br>• asome kifungu kuhusu suala lengwa kwenye kitabu au kwenye tarakilishi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• ajibu maswali kutokana na kifungu husika<br>• atoe muhtasari wa kifungu alichosoma<br>• atunge sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika kifungu, akiwa peke yake, wawiliwawili au kikundi<br>• asome vifungu mtandaoni kuhusu suala lengwa akisaidiwa na mzazi au mlezi wake<br>• awasilishe kwa wenzake ujumbe alioupata katika vifungu | 1. Unazingatia nini unaposoma kifungu cha hadithi?<br>2. Kusoma kuhusu viungo vya mwili vya ndani kuna umuhimu gani?<br>3. Ni hadithi gani umewahi kuisoma kuhusu viungo vya mwili vya ndani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alivyovisoma. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – anaposhirikiana na wenzake katika kutambua viungo vya mwili vya ndani. Vilevile, anapotunga sentensi akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposoma vifungu mtandaoni.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Masuala mtambuko mbalimbali yanayopatikana katika vifungu (*k.v. masuala ya afya, haki za binadamu, usafi n.k.*). | • Heshima – anaposikiliza wengine wakisoma kifungu na kuheshimu maoni yao katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja – anaposhirikiana na wenzake katika vikundi<br>• Uwajibikaji – anaposoma vifungu mtandaoni na kuwasilisha ujumbe uliomo kwa wenzake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafundisha kusoma kwa ufahamu.<br>• Home science – somo hili hushughulikia sehemu za ndani za mwili. | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake katika jamii kuhusu umuhimu wa kusoma kwa ufahamu.<br>• Kujifunza kutoka kwa wanajamii kuhusu usomaji. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu. | Anatambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu kwa wepesi. | Anatambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu. | Anatambua baadhi ya msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu. | Anatatizika kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu. |
| Kueleza maana ya msamiati lengwa. | Anaeleza kwa ufasaha maana ya msamiati lengwa. | Anaeleza maana ya msamiati lengwa. | Anaeleza maana ya baadhi ya msamiati lengwa. | Ana changamoto kueleza maana ya msamiati lengwa. |
| Kusoma kifungu cha hadithi kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe. | Anasoma kifungu cha hadithi kwa ufasaha na wepesi akizingatia ujumbe. | Anasoma kifungu cha hadithi kwa ufasaha akizingatia ujumbe. | Anasoma sehemu ya kifungu cha hadithi kwa ufasaha akizingatia ujumbe. | Anasoma sehemu ya kifungu cha hadithi bila kuzingatia ujumbe. |
| Kujibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi na urahisi. | Anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu kwa usahihi na kutoa muhtasari. | Anajaribu kujibu baadhi ya maswali ya ufahamu. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Kuandika Insha: Insha ya Wasifu**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maudhui ya insha ya wasifu kwa kuzingatia mada ili kukuza ubunifu<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa ubunifu ili kujenga maelezo yenye kutoa picha dhahiri<br>c) kuchangamkia utunzi wa insha ya wasifu ili kujenga ubunifu. | Mwanafunzi:<br>• asome vielelezo vya insha ya wasifu vilivyoandikwa katika matini mbalimbali au tarakilishi huku akitambua maudhui<br>• ashirikiane na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya wasifu<br>• akishirikiane na wenzake katika vikundi ili kubainisha na kujadili vidokezo vifaavyo vya mada lengwa<br>• ajadili maudhui ya insha ya wasifu kwa kurejelea mada<br>• aonyeshe ubunifu kwa kuandika insha ya wasifu isiyopungua maneno 200 inayohusu mada lengwa (*k.m: Daktari nimpendaye*) kwa kuzingatia, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, kanuni za kisarufi (*k.v. uakifishaji mwafaka na tahajia*) na kwa lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali, tashbihi na nahau alizojifunza awali<br>• akuze umilisi wa ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya wasifu | 1. Je, insha nzuri ya wasifu ina muundo gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika insha ya wasifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kumpa motisha kuandika zaidi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya wasifu.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:**<br>• Umoja wa kijamii – kutokana na kufanya kazi pamoja kwenye vikundi vya wanafunzi kutoka maeneo tofauti.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea mada ya insha. | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – hasa katika shughuli za vikundi.<br>• Maadili mbalimbali kutegemea sifa za wahusika katika insha. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English na Indigenous Languages – Masomo haya yanashughulikia uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake katika jamii kuhusu umuhimu wa uandishi bora katika mawasiliano. Aidha, kujifunza kutokana na habari za wasifu zinazotolewa kuwahusu watu katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili maudhui ya insha ya wasifu kwa kuzingatia mada. | Anajadili maudhui ya insha ya wasifu kwa ubunifu kwa kuzingatia mada. | Anajadili maudhui ya insha ya wasifu kwa kuzingatia mada. | Anajadili baadhi ya maudhui ya insha ya wasifu kwa kuzingatia mada. | Ana changamoto kujadili maudhui ya insha ya wasifu kwa kuzingatia mada. |
| Kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Aina za Maneno:** Vivumishi vya Sifa<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vivumishi vya sifa ili kuvitofautisha na aina zingine za maneno<br>b) kutambua vivumishi vya sifa katika matini mbalimbali ili kuvibainisha<br>c) kutumia vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi<br>d) kufurahia kutumia vivumishi vya sifa katika sentensi au vifungu vya maneno. | Mwanafunzi:<br>• aeleze maana ya vivumishi lengwa kwa kurejelea vitu au watu katika mazingira yake (*k.m.: Mwalimu mzuri, njia ndefu, kijiko kichafu*)<br>• atambue vivumishi vya sifa (*k.v. –zuri, -baya, -refu, -fupi, -ekundu, hodari*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• atambue vivumishi vya sifa katika sentensi<br>• atambue vivumishi vya sifa katika kifungu<br>• aandike sentensi kwa usahihi akitumia vivumishi lengwa akiwa peke yake au katika kikundi<br>• ajaze mapengo kwenye sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia vivumishi lengwa kwenye daftari au kwenye tarakilishi. | Ni maneno gani unayotumia kuelezea sifa za watu au kitu? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – anapojadiliana na wenzake katika vikundi.<br>• Ubunifu – anapotunga sentensi akitumia vivumishi vya sifa.<br>• Ujuzi wa kidijitali – anapotumia tarakilishi kutambua vivumishi vya sifa. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za darasani.<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anapojitegemea kujibu maswali darasani. | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – anaposikiliza wengine wakitoa mchango wao darasani.<br>• Uwajibikaji – anapofuata maelekezo ya mwalimu na wenzake darasani. Pia anapotunga sentensi kama alivyoagizwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English language na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya vivumishi. | **Mapendekezo ya Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anapotumia vivumishi vya sifa kwenye mawasiliano ya kila siku katika jamii na pia anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya vivumishi vya sifa. | Anaeleza maana ya vivumishi vya sifa kwa ufasaha na wepesi. | Anaeleza maana ya vivumishi vya sifa kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya vivumishi vya sifa. | Anaeleza maana ya baadhi ya vivumishi vya sifa. |
| Kutambua vivumishi vya sifa katika matini | Anatambua vivumishi vya sifa katika matini | Anatambua vivumishi vya sifa katika matini | Anatambua baadhi ya vivumishi vya sifa katika | Anatambua baadhi ya vivumishi vya sifa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mbalimbali. | mbalimbali kwa wepesi. | mbalimbali. | matini mbalimbali. | katika baadhi ya matini. |
| Kutumia vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi na wepesi. | Anatumia vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatatizika kutumia vivumishi vya sifa kutunga sentensi au vifungu vya maneno. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.2 Aina za Maneno:** Vivumishi Viashiria<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vivumishi viashiria ipasavyo ili kuvibainisha<br>b) kutambua vivumishi viashiria katika matini mbalimbali<br>c) kutumia vivumishi viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi<br>d) kufurahia kutumia vivumishi viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno. | Mwanafunzi:<br>• aeleze maana ya vivumishi lengwa kwa kurejelea vitu vilivyo karibu naye, mbali naye na mbali kabisa (*k.m: Kitabu hiki/hicho/kile*)<br>• atambue vivumishi viashiria (*k.v. huyu, huyo, yule, hivi, hivyo, vile*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno ili kukuza hamu ya ujifunzaji<br>• atambue vivumishi viashiria katika sentensi<br>• atambue vivumishi katika kifungu<br>• aandike sentensi akitumia vivumishi lengwa kwa usahihi wakiwa wawiliwawili au kikundi<br>• ajaze mapengo kwenye sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia vivumishi lengwa<br>• atunge sentensi sahihi au | Ni maneno gani unayoweza kutumia kuonyesha umbali wa mtu au kitu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vifungu vya maneno katika kifaa cha kidijitali akitumia vivumishi lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Hamu ya ujifunzaji – anapotambua vivumishi viashiria katika matini mbalimbali.
- Mawasiliano na ushirikiano – anapojadiliana na wenzake katika vikundi.
- Ubunifu – anapotunga sentensi akitumia vivumishi viashiria.
- Ujuzi wa kidijitali – anapotunga sentensi akitumia kifaa cha kidijitali.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Uraia – anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo mbalimbali katika shughuli za vikundi.<br>• Stadi za maisha – anapojitegemea kujibu maswali darasani. | • Heshima – anaposikiliza wengine wakitoa mchango wao darasani.<br>• Uwajibikaji – anapofuata maelekezo ya mwalimu na wenzake darasani.<br>• Umoja – anapofanya kazi katika vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English, German, French, Chinese na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia mada ya vivumishi. | **Mapendekezo ya Shughuli za Kijamii Zinazochangia Ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anapotumia vivumishi viashiria kwenye mawasiliano ya kila siku katika huduma za kijamii na pia anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi viashiria kutoka kwa wanajamii. |



Not for Sale

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya vivumishi viashiria. | Anaeleza maana ya vivumishi viashiria kwa ufasaha na wepesi. | Anaeleza maana ya vivumishi viashiria kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya vivumishi viashiria. | Anatatizika kueleza maana ya vivumishi viashiria. |
| Kutambua vivumishi viashiria katika matini mbalimbali. | Anatambua vivumishi viashiria katika matini mbalimbali. | Anatambua vivumishi viashiria katika matini mabalimbali. | Anatambua baadhi ya vivumishi viashiria katika matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya vivumishi viashiria katika baadhi ya matini. |
| Kutumia vivumishi viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia vivumishi viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi na wepesi. | Anatumia vivumishi vya viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vya viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatatizika kutumia vivumishi viashiria katika sentensi au vifungu vya maneno. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| 1.4 Sarufi | 1.4.3 Aina za Maneno: Vivumishi Vimilikishi<br><br>(Vipindi 2) | a) Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>b) kuelezea maana ya vivumishi vimilikishi ili kuvitofautisha na aina zingine za vivumishi<br>c) kutambua vivumishi vimilikishi katika matini mbalimbali<br>d) kutumia vivumishi vimilikishi katika sentensi<br>e) kuonea fahari matumizi ya vivumishi vimilikishi katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na mwenzake kueleze maana ya vivumishi vimilikishi ili kuibainisha<br>• atambue vivumishi vimilikishi (*k.v –angu, -ako,*<br>*-ake, -etu, -ao n.k.*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno<br>• atambue vivumishi vimilikishi katika sentensi<br>• atambue vivumishi vimilikishi katika kifungu<br>• ashirikiane na wenzake kujadili katika kikundi au wawiliwawili maana vivumishi vimilikishi huko akitoa mifano<br>• atumie vivumishi vimilikishi katika sentensi kwa kuigiza umiliki wa vitu mbalimbali<br>• atunge sentensi akitumia vivumishi vimilikishi<br>• akuze ujuzi wa kidijitali kwa kutumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi akitumia vivumishi vimilikishi na na kuzituma mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha | Je, unajua maneno yapi yanayotumika kuonyesha kitu ni cha nani? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>ajaze mapengo kwa kutumia vivumishi vimilikishi ili kukamilisha sentensi kwenye daftari au katika tarakilishi kwa kuburura viwakilishi vimilikishi mwafaka.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya vivumishi vimilikishi.</li><li>Hamu ya ujifunzaji - mwanafunzi anapojibu swali dadisi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua vivumishi lengwa.</li><li>Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutumia vivumishi vimilikishi kwa ufasaha katika sentensi.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<ul><li>Uraia – mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali.</li><li>Stadi za maisha – mwanafunzi anapotunga sentensi.</li></ul></td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<ul><li>Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu. Pia mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wengine katika kikundi.</li><li>Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.</li><li>Uwajibikaji - mwanafunzi anapokamilisha kazi yake kwa wakati ufaao.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<ul><li>English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya vivumishi.</li></ul></td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji<ul><li>Mwanafunzi anapotumia vivumishi vimilikishi kwenye mawasiliano ya kila siku katika shughuli za kijamii na pia anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi vimilikishi ya wanajamii.</li></ul></td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuelezea maana ya vivumishi vimilikishi ili kuibainisha. | Anaeleza kwa wepesi maana ya vivumishi vimilikishi. | Anaeleza maana ya vivumishi vimilikishi. | Anajaribu kueleza maana ya vivumishi vimilikishi. | Ana changamoto kueleza maana ya vivumishi vimilikishi. |
| Kutambua vivumishi vimilikishi katika matini mbalimbali. | Anatambua kwa wepesi vivumishi vimilikishi katika matini mbalimbali. | Anatambua vivumishi vimilikishi katika matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya vivumishi vimilikishi katika matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya vivumishi vimilikishi katika baadhi ya matini. |
| Kutumia vivumishi vimilikishi katika sentensi. | Anatumia vivumishi vimilikishi katika sentensi kwa usahihi na wepesi. | Anatumia vivumishi vimilikishi katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vimilikishi katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vimilikishi katika baadhi ya sentensi kwa usahihi. |



Not for Sale

| 2.0 MICHEZO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Maswali Dadisi** |
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili umuhimu maamkuzi na maagano katika mawasiliano<br>b) kujadili maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali<br>c) kutumia aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano<br>d) kuchangamkia maamkuzi na maagano katika mahusiano. | Mwanafunzi:<br>• ajadili na wenzake umuhimu wa maamkuzi na maagano<br>• atambue maamkuzi mbalimbali (*k.v. Waambaje? Salam Aleikum? Unaendeleaje?)* na maagano mbalimbali (*k.v. mchana mwema, buriani, baki salama*) kutoka kwenye chati, ubao, michoro, picha au vifaa vya kidijitali<br>• ashirikiane na mwenzake kujadili maamkuzi na maagano yanayolengwa na matumizi yake<br>• apewe orodha ya maamkuzi na maagano ili kuyaambatanisha na majibu sahihi kwenye tarakilishi<br>• atazame watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali<br>• ashirikiane na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano lengwa na kuheshimu nafasi ya kila mmoja katika maigizo haya<br>• ahusishe mzazi au mlezi wake kutambua maamkuzi na maagano | 1. Kwa nini watu huamkuana?<br>2. Kuagana kuna umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yanayotumiwa katika jamii yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika mchakato wa ujifunzaji.
- Kujiamini – anapotumia na kuigiza maamkuzi na maagano ipasavyo.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Elimu ya amani – maamkuzi na maagano hudumisha amani.<br>• Mshikamano wa kijamii – kupitia kuamkua na kujibu maamkuzi na maagano. | • Heshima – anapoheshimu nafasi za wenzake katika maigizo.<br>• Upendo – maamkuzi na maagano huashiria upendo.<br>• Umoja – anaposhirikiana na wenzake katika kazi za vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia maamkuzi na lugha ya adabu. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>Mwanafunzi awahamasishe wenzake katika jamii kuhusu jinsi ya kuamkua na kuagana ifaavyo na umuhimu wa maamkuzi na maagano. Pia, ajifunze aina mbalimbali za maamkuzi na maagano yanayotumiwa katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili umuhimu wa maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anajadili kwa ufasaha umuhimu wa maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anajadili umuhimu wa maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anajadili baadhi ya hoja kuhusu umuhimu wa maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Ana changamoto kujadili umuhimu wa maamkuzi na maagano katika mawasiliano. |
| Kujadili maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali. | Anajadili kwa ufasaha maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali. | Anajadili maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali. | Anajadili baadhi ya maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali. | Anataja bila kujadili maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali. |
| Kutumia aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anatumia kwa urahisi aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anatumia aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya aina za maamkuzi na maagano katika mawasiliano. | Ana changamoto kutumia maamkuzi na maagano katika mawasiliano. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Kina: Matumizi ya Kamusi (Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maana, tahajia, ngeli na aina za maneno kwa kutumia kamusi<br>b) kutumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za maneno mageni yaliyo katika matini aliyosoma ili kukuza msamiati wake<br>c) kuchangamkia umuhimu wa kamusi katika kukuza msamiati na sarufi ya Kiswahili. | Mwanafunzi:<br>• ashiriki katika mjadala na wenzake kuhusu jinsi ya kutumia kamusi kutambua maana, tahajia, ngeli, aina za maneno na maana za maneno hayo<br>• asikilize msamiati wa suala lengwa (*k.v. kambumbu, gori, hoki, Jugwe)* ukisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kutambua tahajia yake kwa kutumia kamusi akiwa peke yake au katika kikundi<br>• achague maneno kutoka kapu maneno, mti maneno, kadi maneno au kifaa cha kidijitali na kutambua ngeli, aina na maana za maneno hayo kwa kurejelea kamusi akiwa peke yake au katika kikundi.<br>• atumie kamusi kutafuta maana za maneno mbalimbali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• atumie mtandao kutafuta maana za maneno<br>• atumie mtandao kusikiliza na kusoma maelezo kuhusu msamiati anaotafutia maana. | 1. Unatafutaje maana ya maneno kwenye kamusi?<br>2. Kwa nini tunatumia kamusi? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutumia kamusi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia mtandao kutafuta maana za maneno.<br>• Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoanza kutumia kamusi kutafuta maana za maneno.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko:<br>• Stadi za maisha – uwezo wa kujitegemea katika kutumia kamusi.<br>• Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake katika vikundi.</td><td>Uhusiano na Maadili:<br>• Uzalendo – hamu ya kukuza msamiati ili kuweza kutumia lugha ya Kiswahili ipasavyo kama lugha ya taifa.<br>• Upendo – anapotumia kamusi pamoja na wenzake.<br>• Umoja – wanapofanya kazi katika kikundi</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine:<br>• English, German, French, Arabic, Chinese na Indigenous Languages – kamusi hutumika katika mafunzo ya lugha.</td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awahamishe wenzake katika jamii kuhusu umuhimu wa kamusi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.<br>• Ajifunze kutoka kwa wenzake kuhusu matumizi zaidi ya kamusi.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maana, tahajia, ngeli na aina za maneno na kuyatumia ipasavyo. | Anatambua maana, tahajia, ngeli na aina za maneno ipasavyo na kwa urahisi. | Anatambua maana, tahajia, ngeli na aina za maneno ipasavyo. | Anatambua maana, tahajia, ngeli na aina za baadhi ya maneno ipasavyo. | Anatambua maana, tahajia na baadhi ya ngeli na baadhi ya aina za maneno. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za maneno mageni katika matini aliyosoma. | Anatumia kamusi ipasavyo na kwa urahisi kutafuta maana za maneno mageni katika matini aliyosoma. | Anatumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za maneno mageni katika matini aliyosoma. | Anatumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za baadhi ya maneno mageni katika matini aliyosoma. | Anatumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za baadhi ya maneno mageni katika sehemu ya matini aliyosoma. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Kuandika Insha: Insha za Masimulizi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kubainisha vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia mtindo na muundo wake<br>c) kuchangamkia utunzi wa insha ya masimulizi ili kujenga ubunifu. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake katika vikundi ili kubainisha na kujadili vidokezo vifaavyo vya mada lengwa<br>• ashirikiane na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya masimulizi na kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano<br>• atambue insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• aandike insha isiyopungua maneno 200 inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na michezo kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu. Katika kufanya hivi, atakuza ubunifu.<br>• akuze ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya masimulizi mtandaoni na kuisambaza kwa | Je, unazingatia nini ili kuandika insha nzuri ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kidijitali vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea mada ya insha. | • Heshima – hasa katika shughuli za vikundi.<br>• Maadili mbalimbali kutegea tabia za wahusika wa insha. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English na Indigenous Language – masomo haya yanashughulikia uandishi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake katika jamii kuhusu uandishi bora wa masimulizi. Aidha, kujifunza kutokana na masimulizi ya matukio katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubainisha vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi. | Anabainisha kwa ubunifu vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi. | Anabainisha vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi. | Anabainisha baadhi ya vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi. | Anatatizika kubainisha vidokezo vya kutumia katika kuandika insha ya masimulizi. |
| Kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Aina za Maneno:** Vivumishi vya Idadi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vivumishi vya idadi ili kuvitofautisha na aina nyingine za vivumishi<br>b) kutambua vivumishi vya idadi katika matini<br>c) kutumia vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi<br>d) kufurahia kutumia vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno. | Mwanafunzi:<br>• atambue vivumishi vya idadi (*k.v. moja, ishirini, chache, nyingi*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno.<br>• atambue vivumishi vya idadi katika sentensi<br>• atambue vivumishi vya idadi katika kifungu<br>• aeleze maana ya vivumishi lengwa kwa kurejelea vitu vilivyo katika mazingira yao (*k.m. Kitabu kimoja, kalamu nyingi*)<br>• aandike sentensi akitumia vivumishi lengwa kwa usahihi wakiwa wawiliwawili au katika kikundi<br>• ajaze mapengo kwenye sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia vivumishi lengwa<br>• atunge sentensi sahihi au vifungu vya maneno akitumia vivumishi lengwa. | Ni maneno gani unayotumia kutajia idadi ya vitu? |



Not for Sale

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – anapojadiliana na wenzake katika kikundi.<br>• Ubunifu – anapotunga sentensi akitumia vivumishi vya idadi.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Mshikamano wa kijamii – anaposhirirki katika shughuli za darasani.<br>• Stadi za maisha – anapojitegemea kujibu maswali darasani.</td><td>Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – anaposikiliza wengine wakitoa mchango wao darasani.<br>• Uwajibikaji – anapofuata maelekezo ya mwalimu na wenzake darasani.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English, German, French, Chinese na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya vivumishi.</td><td>Mapendekezo ya Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Mwanafunzi anapotumia vivumishi vya idadi kwenye mawasiliano ya kila siku katika huduma za kijamii.<br>• Anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi vya idadi kutoka kwa wanajamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya vivumishi vya idadi ipasavyo. | Anaeleza maana ya vivumishi vya idadi ipasavyo na kwa urahisi. | Anaeleza maana ya vivumishi vya idadi ipasavyo. | Anajaribu kueleza maana ya vivumishi vya idadi ipasavyo. | Anatatizika kueleza maana ya vivumishi vya idadi ipasavyo. |
| Kutambua vivumishi vya idadi katika matini. | Anatambua vivumishi vya idadi katika matini kwa urahisi. | Anatambua vivumishi vya idadi katika matini. | Anatambua baadhi ya vivumishi vya idadi katika matini. | Anatatizika kutambua vivumishi vya idadi katika matini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi na wepesi. | Anatumia vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vya idadi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi vya idadi katika baadhi ya sentensi au vifungu vya maneno. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.2 Aina za Maneno: Vivumishi Viulizi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vivumishi viulizi ili kuvitofautisha na aina nyingine za vivumishi<br>b) kutambua vivumishi viulizi katika matini<br>c) kutumia vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi<br>d) kufurahia kutumia vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vivumishi viulizi<br>• atambue vivumishi viulizi (*k.v. –pi? gani?*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno<br>• atambue vivumishi viulizi katika sentensi<br>• atambue vivumishi viulizi katika kifungu kifupi<br>• aeleze maana ya vivumishi lengwa kwa kurejelea vitu vilivyo katika mazingira yake (*k.m: Kitabu kipi? Nguo gani?*)<br>• ajaze mapengo kwenye sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia vivumishi lengwa<br>• atunge sentensi sahihi au vifungu vya maneno akitumia vivumishi lengwa katika daftari lake au katika kifaa cha kidijitali<br>• awasilishe sentensi zake darasani ili mwalimu na wenzake wazisahihishe. | Ni maneno gani unayotumia kuulizia swali? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – anapojadiliana na wenzake katika vikundi.<br>• Ubunifu – anapotunga sentensi akitumia vivumishi viulizi.<br>• Hamu ya ujifunzaji – anapotambua vivumishi viulizi katika matini mbalimbali. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – anaposhiriki katika shughuli za darasani.<br>• Stadi za maisha – anapojitegemea kujibu maswali darasani. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – anaposikiliza wengine wakitoa mchango wao darasani.<br>• Uwajibikaji – anapofuata maelekezo ya mwalimu na wenzake darasani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English, German, French, Chinese na Indigenous Languages – masomo haya hufunza vivumishi. | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anapotumia vivumishi viulizi kwenye mawasiliano ya kila siku katika huduma za kijamii. Pia, anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi viulizi kutoka kwa wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya vivumishi viulizi ipasavyo. | Anaeleza maana ya vivumishi viulizi ipasavyo na kwa urahisi. | Anaeleza maana ya vivumishi viulizi ipasavyo. | Anajaribu kueleza maana ya vivumishi viulizi. | Ana changamoto kueleza maana ya vivumishi viulizi. |
| Kutambua vivumishi viulizi katika matini. | Anatambua vivumishi viulizi katika matini kwa urahisi. | Anatambua vivumishi viulizi katika matini. | Anatambua baadhi ya vivumishi viulizi matini. | Ana changamoto kutambua vivumishi viulizi katika matini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatambua vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi na wepesi. | Anatambua vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatambua baadhi ya vivumishi viulizi katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatambua baadhi ya vivumishi viulizi katika baadhi ya sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.3 Aina za Maneno: Kivumishi Kirejeshi (amba-)**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-** ili kuyabainisha<br>b) kutambua kivumishi kirejeshi **amba-** katika matini<br>c) kutumia kivumishi kirejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi<br>d) kufurahia kutumia kivumishi kirejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno. | **Mwanafunzi:**<br>• ashirikiane na wenzake kueleza matumizi ya kivumishi kirejeshi amba- ipasavyo<br>• atambue kivumishi kirejeshi amba- (*k.v. ambaye, ambao, ambacho, ambalo n.k*) katika tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno<br>• atambue kivumishi kirejeshi amba- katika sentensi<br>• atambue kivumishi kirejeshi amba- katika kifungu<br>• aeleze maana ya kivumishi lengwa kwa kurejelea vitu vilivyo katika mazingira yake (*k.m: mgeni ambaye, mlango ambao, kiatu ambacho*)<br>• aandike sentensi akitumia kivumishi lengwa kwa usahihi wakiwa wawiliwawili au kikundi<br>• ajaze mapengo kwenye sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia kivumishi lengwa<br>• atunge sentensi sahihi au vifungu vya maneno akitumia kivumishi lengwa. | Je, unakumbuka aina gani za vivumishi? |



Not for Sale

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – anapojadiliana na wenzake katika vikundi.<br>• Ubunifu – anapotunga sentensi akitumia kivumishi kirejeshi **amba-**. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – anaposhirirki katika shughuli za darasani.<br>• Stadi za maisha – anapojitegemea kujibu maswali darasani. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – anaposikiliza wengine wakitoa mchango wao darasani.<br>• Uwajibikaji – anapofuata maelekezo ya mwalimu na wenzake darasani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English, German, French, Chinese na Indigenous Languages– masomo haya yanashughulikia mada ya sarufi. | **Mapendekezo ya Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anapotumia vivumishi virejeshi kwenye mawasiliano ya kila siku katika shughuli za kijamii. Pia, anapojifunza kutokana na matumizi ya vivumishi virejeshi kutoka kwa wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia Katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-** ipasavyo. | Anaeleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-** ipasavyo na kwa urahisi. | Anaeleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-** ipasavyo. | Anajaribu kueleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-**. | Anatatizika kueleza matumizi ya kivumishi kirejeshi **amba-**. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua kivumishi kirejeshi **amba-** katika matini. | Anatambua kivumishi kirejeshi **amba-** katika matini kwa urahisi. | Anatambua kivumishi kirejeshi **amba-** katika matini. | Anatambua baadhi ya vivumishi virejeshi **amba-** katika matini. | Ana changamoto kutambua kivumishi kirejeshi **amba-** katika matini. |
| Kutumia kivumishi kirejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia kivumishi kirejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi na urahisi. | Anatumia kivumishi kirejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi virejeshi **amba-** katika sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vivumishi virejeshi **amba-** katika baadhi ya sentensi au vifungu vya maneno kwa usahihi. |



Not for Sale

| 3.0 Mahusiano | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Matamshi Bora:**<br><br>Vitendawili<br>Sauti:<br>-d/nd<br>-ch/sh<br>-j/nj<br>-g/ng<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuvibainisha<br>b) kutamka maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili ili kuyatambulisha<br>c) kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kujenga matamshi bora<br>d) kuchangamkia matumizi ya vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi kama njia ya kujenga utamkaji | Mwanafunzi:<br>• atambue vitendawili vyenye maneno ya sauti d/nd, ch/sh, j/nj, g/ng katika chati, ubao au vifaa vya kidijitali *(k.v.: Cha ndani hakitoki nje tena cha nje hakitoki ndani (nyama); chakula kikuu cha mtoto (usingizi)*<br>• atamke maneno yenye sauti lengwa katika vitendawili<br>• ashiriki katika kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana wakiwa wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikilize vitendawili vikitegwa na kuteguliwa kupitia vyombo vya kidijitali.<br>• aandike vitendawili alivyovisikiliza na kuwategea wenzake darasani ili | Je, kwa nini watu hutega na kutegua vitendawili? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | bora wa maneno. | kuelimishana | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili kwenye vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiria kuhusu majibu ya vitendawili.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza vitendawili vikitegwa na kuteguliwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutega na kutegua vitendawili.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – wanafunzi wanaposhiriki katika kazi ya vikundi.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali yanayojitokeza kupitia utegaji na uteguzi wa vitendawili mbalimbali. | • Heshima – mwanafunzi anapoheshimu utegaji na uteguzi wa vitendawili wa wenzake.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia vitendawili. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na watu katika jamii kuhusu uimarishaji wa matamshi bora kupitia utegaji na uteguzi wa vitendawili vyenye uradidi. Pia, ajifunze vitendawili zaidi vyenye uradidi vinavyotumiwa na watu katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua ipasavyo vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatambua ipasavyo na kwa urahisi vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatambua ipasavyo vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatambua ipasavyo baadhi ya vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi. | Anatatizika kutambua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi. |
| Kutamka kwa usahihi maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili. | Anatamka kwa usahihi na wepesi maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili. | Anatamka kwa usahihi maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili. | Anatamka kwa usahihi baadhi ya maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili. | Anatamka bila usahihi baadhi ya maneno yenye sauti zinazokaribiana kimatamshi katika vitendawili. |
| Kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa urahisi. | Anatega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa urahisi na wepesi. | Anatega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa urahisi. | Atega na kutegua baadhi ya vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi kwa urahisi. | Anatega baadhi ya vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kimatamshi na kutegua baadhi yavyo. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Kifungu cha Hadithi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu<br>b) kueleza maana ya msamiati lengwa ili kuubainisha<br>c) kusoma kifungu kwa ufasaha ili kupata ujumbe<br>d) kuonyesha uelewa wa kifungu kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari<br>e) kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika mawasiliano<br>f) kuchangamkia habari au ujumbe kwenye kifungu ili | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati unaotumiwa kuonyesha mahusiano kati ya watu katika jamii (*k.v. sahibu /rafiki/ mwandani, mpenzi, mwana, ndugu, jirani, mwenza*) akitumia kapu maneno, mti maneno au tarakilishi<br>• aeleze maana ya msamiati huu kama unavyotumiwa katika jamii wakati wa mawasiliano<br>• atunge sentensi akitumia msamiati husika, akiwa peke yake, wawiliwawili au kikundi<br>• asome kifungu au mchezo mfupi kwa sauti akipishana zamu na wenzake<br>• ajibu maswali kutokana na kifungu<br>• atoe muhtasari kuhusu kifungu alichosoma<br>• asakure mtandaoni ili kupata vifungu vya suala lengwa na kuvisoma | Kuna umuhimu gani kusoma kuhusu mahusiano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kujenga utamaduni wa usomaji. | • aandike ujumbe alioupata katika vifungu vya mtandaoni na kuwasomea wenzake darasani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – anaposoma kifungu au mchezo mfupi kwa sauti na kupishana nafasi na wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – anapojibu maswali kutokana na kifungu.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotumia msamiati lengwa ipasavyo katika sentensi.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.<br>• Stadi za maisha – anapotumia maneno ya mahusiano kuwarejelea wengine katika jamii. | • Heshima – anaposikiliza wengine wakisoma kifungu au mchezo mfupi.<br>• Upendo – anapowaelekeza wengine kujibu maswali.<br>• Uwajibikaji – anaposakura mtandaoni ili kusoma vifungu na kuwasilisha darasani ujumbe alioupata. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji** |
| • English – somo hili hushughulikia kusoma kwa ufahamu<br>• Social studies – somo hili linashughulikia maswala ya kijamii na mahusiano.<br>• English na Indigenous Languages - masomo haya yanashughulikia kusoma kwa ufahamu. | • Mwanafunzi anaweza kuwahamasisha wenzake kuhusu kusoma na kusimulia alichosoma kama thimbitisho la ufahamu<br>• Kushiriki katika shughuli za kijamii kama vile kuwatembelea watoto mayatima na kushiriki nao katika kusoma vifungu mbalimbali<br>• kujifunza kutoka kwa watoto hao kuhusu ujumbe waliopata katika vifungu walivyovisoma. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu. | Anatambua kwa urahisi msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu. | Anatambua msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu. | Anatambua baadhi ya msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu. | Anatatizika kutambua msamiati wa mahusiano uliotumika katika kifungu. |
| Kueleza maana ya msamiati lengwa ipasavyo. | Anaeleza maana ya msamiati lengwa ipasavyo na kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya msamiati lengwa ipasavyo. | Anaeleza maana ya baadhi ya msamiati lengwa ipasavyo. | Ana changamoto kueleza maana ya msamiati lengwa. |
| Kusoma kifungu kwa ufasaha. | Anasoma kifungu kwa ufasaha na wepesi. | Anasoma kifungu kwa ufasaha. | Anasoma sehemu za kifungu kwa ufasaha. | Anatatizika kusoma kifungu. |
| Kujibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi na urahisi. | Anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu bila usahihi. |
| Kutumia msamiati lengwa kwa ufasaha. | Anatumia msamiati lengwa kwa ufasaha na wepesi. | Anatumia msamiati lengwa kwa ufasaha. | Anatumia baadhi ya msamiati lengwa kwa ufasaha | Anatatizika kutumia msamiati lengwa. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Kuandika kwa Kutumia Tarakilishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina mbalimbali za maandishi ya tarakilishi na ishara zinazotumiwa katika maandishi ya tarakilishi<br>b) kuandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maandishi mbalimbali yaliyotofautishwa katika tarakilishi<br>c) kufurahia utumiaji wa tarakilishi katika kuandika. | Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za maandishi ya tarakilishi (*k.v. chapa koza, italiki na maandishi yaliyopigiwa mstari*) akiwa peke yake, wawilwawili au katika kikundi<br>• ashirikiane na wenzake kutambua ishara zinazotumiwa kutofautisha maandishi akiwa pekee yake au katika kikundi<br>• aandike kwa ubunifu kwenye tarakilishi kifungu cha aya moja ya maneno yasiyopungua 50 kuhusu mahusiano kati ya watu katika jamii<br>• atumie kipanya kuchagua sehemu ya maandishi anayolenga kutofautisha<br>• atumie kipanya kuteua ishara anayotaka kutumia kutofautisha maandishi kama vile ishara ya chapa koza, italiki na kupigia mistari.<br>• aonyeshe ujuzi wa kidijitali kwa kuwatumia wenzake kifungu alichoandika mtandaoni ili wamtolee maoni. | Je, unajua maandishi ya aina gani yanayotumika katika tarakilishi? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua ishara zinazotumiwa kutofautisha maandishi kwenye tarakilishi.</li><li>Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotunga vifungu vya maneno na kuviandika kwenye tarakilishi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika.</li><li>Ubunifu – mwanafunzi anapotunga na kuandika kifungu.</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea mada zinazoshughulikiwa (k.v. mshikamano wa kijamii, haki za binadamu).</td><td>Uhusiano na Maadili<ul><li>Heshima – anapowapatia wenzake nafasi ya kutambua ishara zinazotumiwa kutofautisha maandishi kwenye tarakilishi katika kazi ya vikundi.</li><li>Upendo – anapowaelekeza wengine katika matumizi ya tarakilishi.</li><li>Uwajibikaji – anapotunza tarakilishi anapoitumia.</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<ul><li>English na Science and Technology – masomo haya yana mada kuhusu masuala ya kidijitali.</li></ul></td><td>Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<ul><li>Mwanafunzi awe kielelezo katika matumizi ya tarakilishi miongoni mwa wenzake katika jamii. Aidha, anajifunza kutokana na matumizi ya tarakilishi miongoni mwa watu katika jamii.</li></ul></td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua ishara za kupambanua maandishi na | Anatambua ishara za kupambanua maandishi na kuzitumia kwa usahihi | Anatambua ishara za kupambanua maandishi na kuzitumia kwa | Anatambua baadhi ya ishara za kupambanua maandishi na | Anatambua baadhi ya ishara za kupambanua maandishi na kutumia |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kuzitumia kwa usahihi katika tungo. | na urahisi katika tungo. | usahihi katika tungo. | kuzitumia kwa usahihi katika tungo. | baadhi yazo kwa usahihi katika tungo. |
| Kuandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maandishi mbalimbali yaliyotofautishwa. | Anaandika kwa ubunifu kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maandishi mbalimbali yaliyotofautishwa. | Anaandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maandishi mbalimbali yaliyotofautishwa. | Anaandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia baadhi ya maandishi yaliyotofautishwa. | Anatatizika kuandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maandishi mbalimbali yaliyotofautishwa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Aina za Maneno:** Viwakilishi vya Nafsi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya viwakilishi vya nafsi ili kuvitofautisha na viwakilishi vingine<br>b) kutambua viwakilishi vya nafsi katika matini mbalimbali<br>c) kutumia viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika sentensi<br>d) kuonea fahari matumizi ya viwakilishi vya nafsi katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya viwakilishi vya nafsi huko akitoa mifano<br>• atambue viwakilishi vya nafsi (*k.v. mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao, n.k.*) katika ubao, tarakilishi, kapu la maneno au mti wa maneno<br>• atambue viwakilishi vya nafsi katika sentensi<br>• atambue viwakilishi vya nafsi katika kifungu kifupi<br>• atumie viwakilishi vya nafsi kutunga sentensi kwenye daftari au tarakilishi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viwakilishi vya nafsi ili kukamilisha sentensi kwenye daftari au katika tarakilishi. | Je, ni maneno yapi yanayotumika kuwakilisha nafsi mbalimbali? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya viwakilishi vya nafsi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi au kujaza mapengo.<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutumia viwakilishi vya nafsi. | | | | |



Not for Sale

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – anaposhiriki katika shughuli za vikundi.<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anapotunga sentensi | • Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.<br>• Uwajibikaji – Wanafunzi wanapokamilisha kazi yao. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia viwakilishi vya nafsi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anapotumia viwakilishi vya nafsi kwenye mawasiliano ya kila siku katika shughuli za kijamii. Pia, anapojifunza kutokana na matumizi ya viwakilishi nafsi kutoka kwa wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuelezea maana ya viwakilishi vya nafsi kwa usahihi. | Anaeleza maana ya viwakilishi vya nafsi kwa usahihi na kutoa mifano mwafaka. | Anaeleza maana ya viwakilishi vya nafsi kwa usahihi. | Anajaribu kueleza maana ya viwakilishi vya nafsi. | Ana changamoto kueleza maana ya viwakilishi vya nafsi. |
| Kutambua viwakilishi vya nafsi katika matini. | Anatambua viwakilishi vya nafsi katika matini kwa wepesi. | Anatambua viwakilishi vya nafsi katika matini. | Anatambua baadhi ya viwakilishi vya nafsi katika matini. | Anatambua baadhi ya viwakilishi vya nafsi katika baadhi ya matini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia viwakilishi vya nafsi kwa usahihi na urahisi katika sentensi. | Anatumia viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika baadhi ya sentensi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.2 Aina za Maneno:** Viwakilishi Viashiria (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya viwakilishi viashiria ili kuvibainisha<br>b) kutambua viwakilishi viashiria katika matini mbalimbali<br>c) kutumia viwakilishi viashiria kwa usahihi katika sentensi<br>d) kuonea fahari matumizi ya viwakilishi viashiria katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya viwakilishi viashiria huko akitoa mifano mwafaka<br>• atambue viwakilishi viashiria (*k.v. hapa/hapo/pale, huku/huko/kule*) katika ubao, kifaa cha kidijitali, chati, mti wa maneno au kadi za maneno<br>• atambue viwakilishi viashiria katika sentensi<br>• atambue viwakilishi viashiria katika kifungu kifupi<br>• atunge sentensi akitumia viwakilishi viashiria<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viwakilishi viashiria ili kukamilisha sentensi kwenye daftari au katika tarakilishi. | Je, unajua maneno yapi yanayotumika kuonyesha umbali wa kitu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya viwakilishi viashiria.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapotafuta jibu la swali dadisi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi au kujaza mapengo.
- Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutumia viwakilishi viashiria katika sentensi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – kushiriki katika vikundi.<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anapotunga sentensi. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.<br>• Uwajibikaji – wanafunzi wanapokamilisha kazi yao. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia viwakilishi viashiria. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anaweza kuwa kielelezo bora katika kutumia viwakilishi viashiria. Pia, anajifunza kutokana na matumizi ya viwakilishi viashiria kutoka kwa wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya viwakilishi viashiria kwa usahihi. | Anaeleza maana ya viwakilishi viashiria kwa usahihi na kutoa mifano mwafaka. | Anaeleza maana ya viwakilishi viashiria. | Anajaribu kueleza viwakilishi viashiria. | Anatatizika kueleza maana ya viwakilishi viashiria. |
| Kutambua viwakilishi viashiria katika matini mbalimbali. | Anatambua viwakilishi viashiria katika matini kwa wepesi. | Anatambua viwakilishi viashiria katika matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya viwakilishi viashiria katika matini. | Anatambua baadhi ya viwakilishi viashiria katika baadhi ya matini. |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia viwakilishi viashiria kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia viwakilishi viashiria kwa usahihi na urahisi katika sentensi. | Anatumia viwakilishi viashiria kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya viwakilishi viashiria kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya viwakilishi viashiria kwa usahihi katika baadhi ya sentensi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.3 Aina za Maneno: Viwakilishi vya Idadi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya viwakilishi vya idadi ili kuvitofautisha na viwakilishi vingine<br>b) kutambua viwakilishi vya idadi katika matini mbalimbali<br>c) kutumia viwakilishi vya idadi kwa usahihi katika sentensi ili kuboresha mawasiliano<br>d) kuonea fahari matumizi ya viwakilishi vya idadi katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya viwakilishi vya idadi huko akitoa mifano mwafaka<br>• atambue viwakilishi vya idadi (*k.v. chache, nyingi, tatu, kumi n.k.)* katika ubao, kadi za maneno, chai, mti wa maneno, chati au kifaa cha kidijitali<br>• atambue viwakilishi vya idadi katika sentensi<br>• atambue viwakilishi vya idadi katika kifungu kifupi<br>• atumie viwakilishi vya idadi kutunga sentensi daftarini au katika kifaa cha kidijitali<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viwakilishi viashiria ili kukamilisha sentensi kwenye daftari au katika kifaa cha kidijitali. | Je, unajua maneno yapi yanayotumika kuonyesha idadi ya vitu? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya viwakilishi vya idadi.<br>• Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojibu swali dadisi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi au kujazia mapengo<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutumia viwakilishi vya idadi. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – kushiriki katika vikundi.<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anapotunga sentensi. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.<br>• Uwajibikaji – Wanafunzi wanapokamilisha kazi yao. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya viwakilishi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anaweza kuwa kielelezo bora katika kutumia viwakilishi vya idadi. Aidha, anajifunza kutokana na matumizi ya viwakilishi vya idadi kutoka kwa wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya viwakilishi kwa usahihi. | Anaeleza maana ya viwakilishi vya idadi kwa usahihi na wepesi. | Anaeleza maana ya viwakilishi vya idadi kwa usahihi. | Anajaribu kueleza maana ya viwakilishi vya idadi. | Ana changamoto kueleza maana ya viwakilishi vya idadi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viwakilishi vya idadi katika matini. | Anatambua viwakilishi vya idadi katika matini kwa urahisi. | Anatambua viwakilishi vya idadi katika matini. | Anatambua baadhi ya viwakilishi vya idadi katika sentensi. | Anatambua baadhi ya viwakilishi vya idadi katika baadhi ya matini. |
| Kutumia viwakilishi vya idadi katika sentensi<br>kwa usahihi. | Anatumia viwakilishi vya idadi katika sentensi kwa usahihi na wepesi. | Anatumia viwakilishi vya idadi katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya viwakilishi vya idadi katika sentensi kwa usahihi i. | Anatumia baadhi ya viwakilishi vya idadi kwa usahihi katika baadhi ya sentensi. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.4 Uakifishi**<br><br>**Alama ya hisi (!)**<br>**Ritifaa (')**<br>**Koloni (:)**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi<br>b) kutumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika maaandishi<br>c) kufurahia matumizi ya alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi. | Mwanafunzi:<br>• atambue alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi<br>• ashiriki katika vikundi kuakifisha sentensi akitumia alama ya hisi, ritifaa na koloni<br>• ashiriki katika vikundi kuakifisha kifungu kifupi akitumia alama ya hisi, ritifaa na koloni<br>• aandike sentensi akitumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika daftari lake<br>• aandike sentensi zenye alama ya hisi, ritifaa na koloni akitumia kifaa cha kidijitali. | 1. Kwa nini alama za kuakifisha hutumiwa katika maandishi?<br>2. Ni alama gani za uakifishi unazoweza kuzitumia kwa usahihi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki mijadala kuhusu uakifishi.
- Ubunifu – wanapotunga sentensi wakitumia viakifishi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kuakifisha sentensi au vifungu ifaavyo.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Uraia – kutunga sentensi zinazolenga uraia mwema.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali yanayojitokeza katika sentensi mbalimbali | • Umoja – kufanya kazi katika makundi.<br>• Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wengine katika kikundi. |

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji: |
|---|---|
| • English na Indigenous Language - masomo haya hushughulikia uakifishi. | • Mwanafunzi atakuwa kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha katika jamii. Ataweza pia kujifunza kutokana na uakifishi uliotumika katika matini mbalimbali zinazotumika katika shughuli za kila siku. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi. | Anatambua kwa urahisi alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi. | Anatambua alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi. | Anatambua alama ya hisi, ritifaa na koloni katika baadhi ya maandishi. | Ana changamoto kutambua alama ya hisi, ritifaa na koloni katika maandishi. |
| Kutumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika maandishi. | Anatumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo na kwa wepesi katika maandishi. | Anatumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika maandishi. | Anatumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika baadhi ya maandishi. | Ana changamoto kutumia alama ya hisi, ritifaa na koloni ifaavyo katika maandishi. |

| 4.0 MISIMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Heshima, Adabu na Vyeo: Maneno ya Heshima**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima yanayotumiwa katika mawasiliano<br>b) kuonyesha uelewa wa maneno ya heshima kwa kuyatumia kwa usahihi katika mawasiliano<br>c) kuthamini kutumia maneno ya heshima katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi:<br>• atambue maneno ya heshima (*k.v. shehe, kasisi, padre, mwadhini, mheshimiwa, rais, mtawa*) kwenye ubao, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno<br>• aeleze maana ya maneno lengwa kama yanavyotumiwa katika mahusiano ya kila siku kati ya watu<br>• atunge sentensi kwa kutumia maneno lengwa kwa usahihi<br>• atazame maigizo ya watu wakitumia maneno ya heshima kwenye tarakilishi na video<br>• aigize mazungumzo mafupi akiwa na wenzake huku akitumia msamiati wa heshima.<br>• asaidiwe na mzazi na mlezi wake katika kutambua maneno ya heshima yanayotumiwa katika jamii. | 1. Ni maneno yapi ya heshima unayoyajua na unayoweza kutumia kurejelea watu tofauti?<br>2. Kutumia maneno ya heshima kuna umuhimu gani katika jamii? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Ujuzi wa kidijitali – anapotumia tarakilishi, video na projekta kutazama maigizo mafupi.<br>• Mawasiliano na ushirikiano – anaposhiriki katika maigizo na mijadala.<br>• Kujiamini – anapoigiza ipasavyo mazungumzo akitumia msamiati wa heshima. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – anaposhiriki katika maigizo mafupi akiwa na wenzake.<br>• Masuala ya kiuana – anapotumia maneno yanayorejelea uana mahususi katika mawasiliano. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – anapotumia maneno ya udugu. Pia anapoheshimu nafasi za wenzake katika maigizo.<br>• Upendo – anapotumia maneno ya udugu kwa wenzake na kwa wakubwa wake.<br>• Uwajibikaji – anapotumia maneno ya heshima kuwarejelea watu maalum. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• Religious Education – Somo hili hushughulikia maadili ya heshima.<br>• English Language – somo hili hushughulikia matumizi ya lugha ya heshima katika mawasiliano. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake katika jamii kuhusu umuhimu wa kutumia lugha ya heshima wanapowasiliana na watu wengine. Pia ajifunze maneno zaidi ya heshima yanayotumiwa katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maneno ya heshima | Anatambua maneno ya heshima yanayotumiwa | Anatambua maneno ya heshima | Anatambua baadhi ya maneno ya heshima | Anatatizika kutambua maneno ya heshima |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| yanayotumiwa katika mawasiliano. | katika mawasiliano kwa urahisi. | yanayotumiwa katika mawasiliano. | yanayotumiwa katika mawasiliano. | yanayotumiwa katika mawasiliano. |
| Kutumia maneno ya heshima kwa usahihi katika mawasiliano. | Anatumia maneno ya heshima kwa usahihi na kwa wepesi katika mawasiliano. | Anatumia maneno ya heshima kwa usahihi katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya maneno ya heshima kwa usahihi katika mawasiliano. | Ana changamoto kutumia maneno ya heshima katika mawasiliano. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Mapana:** Matini ya Kidijitali (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali anaposoma<br>b) kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma vyenye mada lengwa<br>c) kutumia vifaa ya kidijitali kwa urahisi ili kupata matini yanayolengwa<br>d) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | Mwanafunzi:<br>• ajadili na wenzake kuhusu hatua za kiusalama na maadili anayofaa kuzingatia anapotafuta na kusoma matini ya kidijitali<br>• ajadili na wenzake kuhusu utunzaji wa vifaa vya kidijitali anavyotumia katika usomaji<br>• azingatie hatua za kiusalama katika kutumia vifaa vya kidijitali (*k.v. kufungua mitandao ifaayo*)<br>• atambue jina la faili lengwa kwenye tarakilishi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga faili<br>• atambue mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake<br>• atambue umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao<br>• asome matini yanayojumuisha msamiati wa misimu kwa kutumia vifaa vya kidijitali | Kusoma matini ya kidijitali kuna manufaa gani? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • atafute maana za maneno mapya kwenye kamusi mtandaoni<br>• asikilize matamshi na maelezo kuhusu anachokisoma mtandaoni panapowezekana<br>• atoe habari kwa muhtasari kuhusu matini aliyosoma na kujibu maswali katika maandishi au mazungumzo na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia katika kutafuta, kusakura na kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi atapata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Stadi za maisha – ujuzi wa kidijitali na usalama mitandaoni. | • Uwajibikaji – katika utunzaji wa vifaa vya kidijitali na kuzingatia mitandao salama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• Masomo yote huzingatia matumizi ya vifaa vya kidijitali. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuweza kuwahamasisha wenzake katika jamii na shuleni kuhusu misimu mbalimbali na jinsi ya kujiandaa kwa misimu hiyo. Kujifunza kutokana na wanajamii kuhusu misimu. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|

| **Vigezo** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali anaposoma. | Anatambua hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kila mara anaposoma. | Anatambua hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali anaposoma. | Anatambua baadhi ya hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali anaposoma. | Anatambua baadhi ya hatua za kiusalama katika matumizi ya baadhi ya vifaa vya kidijitali. |
| Kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. | Anasakura matini kwenye tovuti salama kila mara ili kupata vifungu vya kusoma | Anasakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. | Anajaribu kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. | Anasakura baadhi ya matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. |
| Kutumia vifaa vya kidijitali kwa urahisi ili kupata matini. | Anatumia vifaa vya kidijitali kwa urahisi na kwa ukakamavu ili kupata matini. | Anatumia vifaa vya kidijitali kwa urahisi ili kupata matini. | Anatumia baadhi ya vifaa vya kidijitali kwa urahisi ili kupata matini. | Ana changamoto kutumia vifaa vya kidijitali ili kupata matini. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Aina za Insha: Barua Rasmi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake<br>b) kutambua vipengele vya barua rasmi ili kuvizingatia katika uandishi<br>c) kuandika barua rasmi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>d) kuchangamkia umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue barua rasmi kwenye kielelezo cha barua rasmi iliyochapishwa au kwenye tarakilishi<br>• ashirikiane na wenzake kujadili vipengele vya barua rasmi (*k.v. anwani ya mwandishi [jina, sanduku la posta, tarehe], anwani ya mpokeaji [cheo, sanduku la posta], mtajo, mada ya barua, mwili, hitimisho, sahihi* na *jina la mwandishi)*<br>• aandike barua rasmi kwa mwalimu akiomba kujiunga na klabu shuleni (*k.v. vile skauti, kilimo na muziki*), akishirikiana na wenzake darasani, kwa hati za mkono au kwa kutumia kifaa cha kidijitali akizingatia muundo wa uandishi wa barua rasmi<br>• aandike barua rasmi katika daftari akiwa peke yake<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano. | 1. Barua rasmi ni gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika barua rasmi? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa** | |
|---|---|
| <ul><li>Mawasiliano na ushirikiano – anaposhirikiana na wenzake kujadili barua rasmi.</li><li>Ubunifu – anapotunga na kuandika barua rasmi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali – anapoandika barua kwa kutumia kifaa cha kidijitali.</li><li>Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – anapowaza kuhusu kanuni za barua rasmi na kupanga aya.</li></ul> | |
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<ul><li>Stadi za maisha – anapotumia barua rasmi kuwasiliana.</li><li>Masuala mtambuko mbalimbali kuhusiana na mada ya barua rasmi.</li></ul> | **Uhusiano na Maadili**<ul><li>Umoja – wanaposhirikiana kujadili vipengele vya barua rasmi.</li><li>Heshima – anapozingatia maoni ya ya wengine wakati wa mijadala.</li><li>Uwajibikaji – anapoandika barua rasmi kama anavyoagizwa.</li></ul> |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<ul><li>English – Somo hili hushughulikia uandishi wa barua rasmi</li></ul> | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<ul><li>Mwanafunzi ashiriki katika uandishi wa barua rasmi katika jamii kama vile katika vikundi vya kijamii. Aidha, anajifunza kutokana na barua rasmi anazotangamana nazo shuleni au nje ya shule.</li></ul> |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake. | Anatambua kwa urahisi barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake. | Anatambua barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake. | Anatambua baadhi ya barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake. | Anatatizika kutambua barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vipengele vya barua rasmi. | Anatambua kwa urahisi vipengele vya barua rasmi. | Anatambua vipengele vya barua rasmi. | Anatambua baadhi ya vipengele vya barua rasmi. | Ana changamoto kutambua vipengele vya barua rasmi. |
| Kuandika barua rasmi ipasavyo kwa kuzingatia muundo wake. | Anaandika barua rasmi ipasavyo na kwa wepesi kwa kuzingatia muundo wake. | Anaandika barua rasmi ipasavyo kwa kuzingatia muundo wake. | Anaandika barua rasmi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake vya kimuundo. | Anatatizika kuandika barua rasmi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4. Umoja na Wingi wa Nomino: Ngeli ya YA-YA**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za ngeli ya YA-YA katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya YA-YA<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya YA-YA katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya YA-YA kwenye kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.m. maji, maziwa, mate, marashi na maskani)*<br>• aandike nomino katika ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya YA-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya YA-YA kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | Je, unajua majina gani ya vitu visivyohesabika? |



Not for Sale

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.</li><li>Kujiamini – mwanafunzi anapotumia nomino za ngeli ya YA-YA ipasavyo.</li><li>Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua nomino na ngeli zake.</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<ul><li>Mshikamano wa kijamii – wanapofanya kazi kwa vikundi.</li><li>Stadi za Maisha – wanapojifanyia kazi darasani.</li></ul></td><td>Uhusiano na Maadili<ul><li>Uwajibikaji – kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.</li><li>Umoja – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<ul><li>English na Indigenous Languages – masomo haya yanajumuisha mada za sarufi.</li></ul></td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<ul><li>Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. Anajifunza kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii.</li></ul></td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino katika ngeli ya YA-YA katika matini. | Anatambua kwa urahisi nomino katika ngeli ya YA-YA katika matini. | Anatambua nomino katika ngeli ya YA-YA katika matini. | Anatambua baadhi ya nomino katika ngeli ya YA-YA katika matini. | Ana changamoto kutambua nomino katika ngeli ya YA-YA katika matini. |
| Kuandika nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi. | Anaandika kwa urahisi nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi. | Anaandika nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi. | Anaandika baadhi ya nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi. | Anatatizika kuandika nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya YA-YA. | Anaandika kwa urahisi umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya YA-YA. | Anaandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya YA-YA. | Anaandika umoja na wingi wa mafungu ya baadhi ya maneno katika ngeli ya YA-YA. | Ana changamoto kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya YA-YA. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.2 Umoja na Wingi wa Sentensi: Ngeli ya YA-YA**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya nomono za ngeli ya YA-YA katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya YA-YA katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya YA-YA katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikilize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya YA-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi sahihi kwa kutumia nomino za ngeli ya YA-YA akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya YA-YA kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | Je, unajua majina gani ya vitu ambayo hayabadiliki katika umoja na wingi? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi.<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutunga sentensi sahihi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua nomino na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda. | | | | |

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – anapofanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha –- anapojifanyia kazi darasani<br>• Masuala mtambuko anuwai kutokana na sentensi zinazoundwa. | • Uwajibikaji – anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.<br>• Uzalendo – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza ngeli | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. Pia atajifunza kutokana na matumizi ya lugha ya watu mbalimbali katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi. | Anatambua kwa wepesi viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi. | Anatambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye baadhi ya sentensi. |
| Kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi kwa urahisi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anaunda baadhi ya sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anaunda baadhi ya sentensi akitumia baadhi ya nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. |

| 5.0 MSHIKAMANO WA KITAIFA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Methali:** Methali Zinazohusu Umoja na Ushirikiano<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini<br>b) kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano katika jamii<br>c) kutumia methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano<br>d) kuchangamkia matumizi ya methali zinazohimiza umoja na ushirikiano. | Mwanafunzi:<br>• atambue methali zinazohusu umoja na ushirikiano (*kama vile; umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, jifya moja haliinjiki chungu, kidole kimoja hakivunji chawa, kinga na kinga ndio moto huwaka n.k.*) katika chati, ubao na vyombo vya kidijitali<br>• atoe mifano ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika jamii<br>• asikilize methali za umoja na ushirikiano zikitumiwa kupitia vyombo vya kidijitali<br>• ajadili na wenzake maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano<br>• alinganishe methali na maana yake<br>• akamilishe methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mazungumzo akishirikiana na wenzake, kwenye daftari au kwa kutumia vyombo vya kidijitali | 1. Je, ni nini umuhimu wa methali katika jamii?<br><br>2. Ni methali gani unazozijua kuhusu umoja na ushirikiano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • asakure mtandaoni kwa kusaidiwa na mzazi au mlezi wake ili kupata methali zaidi zinazohusu umoja na ushirikiano na matumizi ya methali hizo<br>• ajadili na wenzake kuhusu methali alizozipata mtandaoni ili wajengane kimaarifa. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili methali kwenye vikundi.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiria kuhusu matumizi ya methali.<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapotumia methali kujieleza.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua methali. |

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Ushauri nasaha – methali zinahusu maadili.<br>• Mshikamano wa kijamii – kushiriki katika vikundi. | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake katika kikundi.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia methali. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Awaelekeze watu katika jamii kuhusu umuhimu wa methali na kujifunza methali zaidi kuhusu umoja na ushirikiano katika lugha mbalimbali. |



Not for Sale

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini. | Anatambua kwa urahisi methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini. | Anatambua methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini. | Anatambua baadhi ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini. | Anatatizika kutambua methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini. |
| Kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano. | Anaeleza kwa ufasaha maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano. | Anaeleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano. | Anaeleza maana na matumizi ya baadhi ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano. | Anaeleza maana za baadhi ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano bila kueleza matumizi yake. |
| Kutumia methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia kwa usahihi na ubunifu methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia kwa usahihi methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia kwa usahihi baadhi ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano bila usahihi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Lugha katika Ushairi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili dhana za ukwapi na utao katika shairi ili kuzibainisha<br>b) kutambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa kuzingatia muundo<br>c) kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia ili kupata ujumbe<br>d) kuchangamkia usomaji wa mashairi ili kuyathamini. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake katika vikundi, kujadili ukwapi na utao katika shairi<br>• atambue ukwapi na utao katika shairi kwenye ubao, chati, vitabu au vyombo vya kidijitali<br>• ashirikiane na wenzake kusoma shairi akizingatia ukwapi na utao<br>• ajirekodi akisoma aina za mashairi lengwa akitumia vyombo vya kidijitali ili kuweza kujirekebisha anakokosea<br>• atofautishe mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwenye ubao, chati, vitabu au vifaa vya kidijitali<br>• atambue mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia katika matini mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa mahadhi mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe kwenye shairi waliyoyasoma<br>• ajibu maswali yanayotokana na mashairi aliyoyasoma<br>• akisaidiana na mzazi au mlezi, asakure mtandaoni ili kusoma mashairi ya tathnia, | Je, kuna tofauti gani kati ya mashairi mbalimbali? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | tathlitha na tarbia<br>• aandike ujumbe alioupata katika mmojawapo wa mashairi aliyoyasoma na kuwasomea wenzake darasani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi kujadili aina lengwa za mashairi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotafakari kuhusu ujumbe wa mashairi aliyosoma mtandaoni.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kusoma mashairi kwa mahadhi yafaayo. Pia anapoweza kufafanua ipasavyo ujumbe wa shairi alililisoma.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua aina za shairi.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kutokana na kushiriki katika vikundi.<br>• Masuala mtambuko anuwai kutokana na maudhui ya mashairi. | • Heshima – mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake katika kikundi.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia ushairi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni kuhusu mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na jinsi yanavyoweza kutumiwa kupasha ujumbe mbalimbali katika jamii. Naye ajifunze kutoka kwa wenzake ujumbe zaidi unaoweza kuwasilishwa kupitia kwa mashairi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili dhana za ukwapi na utao katika shairi ipasavyo. | Anajadili dhana za ukwapi na utao katika shairi ipasavyo na kwa wepesi. | Anajadili dhana za ukwapi na utao katika shairi ipasavyo. | Anajaribu kujadili dhana za ukwapi na utao katika shairi. | Anatatizika kujadili dhana za ukwapi na utao katika shairi |
| Kutambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia | Anatambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa urahisi. | Anatambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia. | Anatambua baadhi ya mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia. | Anatatizika kutambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia. |
| Kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na kueleza ujumbe uliomo. | Anasoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na kueleza ujumbe uliomo kwa ufasaha. | Anasoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na kueleza ujumbe uliomo. | Anasoma baadhi ya mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na kueleza ujumbe uliomo. | Anasoma baadhi ya mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia na kueleza sehemu ya ujumbe uliomo. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Kuandika Insha: Insha za Maelezo**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze,<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi bora maishani. | Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili vidokezo vya insha ya maelezo atakavyovitumia katika kuandika insha yake<br>• aonyeshe umilisi wa ubunifu kwa kuandika insha ya maelezo (*k.v. Siku ya sherehe ya kitaifa, Siku ya michezo ya kitaifa, Nchi yetu, n.k*) isiyopungua maneno 200 akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali na nahau alizojifunza awali ili kutoa picha dhahiri kuhusu anachokielezea<br>• akuze umilisi wa ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya maelezo na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini. | Insha ya maelezo ina sifa gani? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.<br>• Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia – kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea mada ya insha.</td><td>Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima – hasa katika shughuli za vikundi.<br>• Uwajibikaji – mwanafunzi anapowajibika kuandika insha ifaavyo.<br>• Umoja – wanafunzi wanapojadiliana pamoja.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigenous Language – masomo haya yanajumuisha uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha.</td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwahamasisha wenzake katika jamii kuhusu umuhimu wa uandishi bora wa maelezo katika mawasiliano. Vilevile, atajifunza kutokana na maelezo yanayotolewa na wanajamii katika shughuli za kila siku.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua insha za maelezo katika matini. | Anatambua kwa urahisi insha za maelezo katika matini. | Anatambua insha za maelezo katika matini. | Anatambua baadhi ya insha za maelezo katika matini. | Ana changamoto kutambua insha za maelezo katika matini. |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya maelezo yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo akizingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Anaandika insha ya maelezo iakizingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo akizingatia baadhi ya kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo bila kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio wa mawazo. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Umoja na Wingi wa Nomino: Ngeli ya U-U (Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya U-U katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya U-U<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-U katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U (*k.m: uji, ugali, uhuru, ujanja, urafiki*) kwenye kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U katika sentensi<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U katika kifungu kifupi<br>• aandike daftarini mwake nomino katika ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya U-U kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya U-U kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya U-U ? |



Not for Sale

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapotambua nomino za ngeli ya U-U ipasavyo.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua nomino za ngeli ya U-U.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Mshikamano wa kijamii – wanapofanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha – wanapojifanyia kazi darasani</td><td>Uhusiano na Maadili<br>• Uwajibikaji – kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Uzalendo – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya nomino</td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. Pia, atajifunza kutokana na matumzi ya lugha ya wanajamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino katika ngeli ya U-U katika matini. | Anatambua nomino katika ngeli ya U-U na matini. | Anatambua nomino katika ngeli ya U-U katika matini. | Anatambua baadhi ya nomino katika ngeli ya U-U katika matini. | Ana changamoto kutambua nomino katika ngeli ya U-U katika matini. |
| Kuandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi. | Anaandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi kwa urahisi. | Anaandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi. | Anaandika baadhi ya nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi. | Anatatizika kuandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya U-U | Anaandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya U-U kwa urahisi. | Anaandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya U-U. | Anaandika umoja na wingi wa baadhi ya mafungu ya maneno katika ngeli ya U-U. | Ana changamoto kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya U-U. |



Not for Sale

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.2 Umoja na Wingi wa Sentensi:** Ngeli ya U-U (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya U-U katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya U-U katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya U-U katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya U-U kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya U-U akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-U kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | Je, unakumbuka nomino zipi ambazo zinaanza kwa herufi U katika umoja? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu atakachoandika.
- Ujuzi wa kidijitali – kutumia tarakilishi kutambua nomino na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kufanya kazi kwa vikundi.<br>• Stadi za Maisha – anapojifanyia kazi darasani. | • Uwajibikaji – kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Umoja – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia ngeli. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. Pia, atajifunza kutokana na matumzi ya lugha ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi. | Anatambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi kwa urahisi. | Anatambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye baadhi ya sentensi. |
| Kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi kwa urahisi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia baadhi ya nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. |



Not for Sale

| 6.0 USAWA WA KIJINSIA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora: Ushairi**<br><br>**Sauti lengwa:**<br>**-d/nd**<br>**-ch/sh**<br>**-j/nj**<br>**-g/ng)**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kukariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali ili kukuza matamshi bora.<br>b) kueleza maana ya maneno yenye sauti lengwa yaliyotumika katika shairi<br>c) kutumia kwa usahihi msamiati uliotumiwa katika shairi kuboresha mawasiliano<br>d) kuonyesha ufahamu wa ujumbe katika shairi kwa kujibu maswali kuchangamkia mahadhi mbalimbali katika ushairi. | Mwanafunzi:<br>• asikilize shairi kuhusu suala lengwa na lenye maneno yenye sauti lengwa (**d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng**) likikaririwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali<br>• akariri akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali<br>• atamke maneno yaliyoundwa kutokana na sauti d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng katika shairi<br>• atambue msamiati uliotumika katika ushairi kuhusu usawa wa kijinsia (*k.m. jinsia, ubaguzi, mtoto wa kiume, mtoto wa kike, usawa, heshima na uwajibikaji*)<br>• atumie msamiati uliotumika katika shairi kutunga sentensi sahihi akiwa peke yake, wawili wawili au | Kwa nini kusoma na kukariri mashairi ni muhimu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | katika vikundi<br>• asakure mtandaoni, akishirikiana na wenzake, ili kukariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe katika shairi walililiimba<br>• ajibu maswali yanayotokana na shairi alilosikiliza, aliloimba au kukariri.<br>• aendelee kusoma mashairi katika vitabu na mtandaoni ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anasikiliza shairi lililorekodiwa likikaririwa. Pia, anaposakura mtandaoni kupata mashairi zaidi na kuyakariri.
- Kujiamini – mwanafunzi anapokariri shairi kwa kuzingatia matamshi bora na mahadhi mbalimbali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kusoma mashairi katika vitabu na mtandaoni.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko: | Uhusiano na Maadili: |
|---|---|
| • Masuala mtambuko mbalimbali yaliyoshughulikiwa katika mashairi (*k.m. haki na usawa wa kijinsia*, *mshikamano wa kijamii*, *masuala ya afya*). | • Shairi kuhusu maadili lizingatie masuala tofauti ya uadilifu k.v. heshima, upendo, adabu na uaminifu |

| **Uhusiano na Masomo Mengine:** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
|---|---|
| • English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia ushairi. | • Mwanafunzi atawahamasisha wenzake shuleni na kijijini kuhusu umuhimu wa usawa wa kijinsia.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kukariri na kuimba mashairi yenye ujumbe ili kuwahamasisha watu kuhusu masuala mbalimbali. Pia ajifunze mahadhi mbalimbali yanayotumiwa katika jamii katika ukariri wa mashairi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kukariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali. | Anakariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali kwa ufasaha. | Anakariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali. | Anakariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia baadhi ya matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali. | Anakariri au kuimba baadhi ya sehemu za shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia baadhi ya matamshi ya maneno yenye sauti lengwa. |
| Kueleza maana ya maneno yenye sauti lengwa | Anaeleza kwa ufasaha na urahisi maana ya maneno yenye sauti | Anaeleza kwa ufasaha maana ya maneno yenye sauti | Anaeleza kwa ufasaha baadhi ya maana ya maneno yenye sauti | Anatatizika kueleza maana ya maneno yenye sauti lengwa yaliyotumika katika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| yaliyotumika katika shairi. | lengwa yaliyotumika katika shairi. | lengwa yaliyotumika katika shairi. | lengwa yaliyotumika katika shairi. | shairi. |
| Kutumia kwa usahihi msamiati uliotumiwa katika shairi. | Anatumia kwa usahihi na urahisi msamiati uliotumiwa katika shairi. | Anatumia kwa usahihi msamiati uliotumiwa katika shairi. | Anatumia kwa usahihi baadhi ya msamiati uliotumiwa katika shairi. | Ana changamoto kutumia kwa usahihi msamiati uliotumiwa katika shairi. |



Not for Sale

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Mapana:** Makala<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba<br>b) kutambua makala atakayosoma katika maktaba<br>c) kusoma makala mbalimbali ili kupata ujumbe<br>d) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi:<br>• aeleze umuhimu wa kusoma kwa mapana<br>• ajadili mambo ya kuzingatia anapochagua matini za kusoma katika maktaba (*k.v. makala yanayoambatana na umri, ukubwa wa maandishi, ujumbe anaotaka kuupata*)<br>• achague makala mbalimbali kuhusu suala lengwa katika maktaba (makala yaliyochapishwa au katika kifaa cha kidijitali)<br>• asome makala ya aina mbalimbali aliyoyachagua<br>• ajadiliane kwa heshima na wenzake kuhusu ujumbe alioupata katika makala aliyoyasoma atumie kamusi kupata maana za msamiati uliotumika katika makala. | 1. Je, kwa nini ni muhimu kuwa na mazoea ya kusoma makala au hadithi?<br>2. Kusoma makala kuhusu usawa wa kijinsia kuna umuhimu gani? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika vikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposoma makala katika vifaa vya kidijitali.<br>• Kujiamini – anaposoma makala mbalimbali na kuweza kueleza ujumbe uliomo. | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:**<br>• Stadi za maisha – uwezo wa kuongoza na kuelekeza usomaji wake.<br>• Ushauri nasaha – anaposoma masuala ya kijinsia katika matini anayosoma. | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – anapojadiliana na wenzake kuhusu ujumbe ulio katika makala.<br>• Umoja – anaposhirikiana na wenzake katika kikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English – somo hili linashughulikia kusoma kwa mapana. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni kuhusu umuhimu wa kusoma na mapana.<br>• Ajifunze kutoka kwa wenzake kuhusu baadhi ya makala waliyofaidika nayo. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba. | Anajadili kwa urahisi mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba. | Anajadili mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba. | Anajadili baadhi ya mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba. | Anatatizika kujadili mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba. |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua makala atakayosoma katika maktaba. | Anatambua kwa wepesi makala atakayosoma katika maktaba. | Anatambua makala atakayosoma katika maktaba. | Anatambua baadhi ya makala atakayosoma katika maktaba. | Ana changamoto kutambua makala atakayosoma katika maktaba. |
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe, vipengele vya makala na kueleza alichokisoma. | Anasoma akizingatia ujumbe, vipengele vya makala na kueleza alichokisoma kwa wepesi. | Anasoma akizingatia ujumbe, vipengele vya makala na anaweza kueleza alichokisoma. | Anasoma akizingatia sehemu za ujumbe, anafahamu baadhi ya vipengele vya makala na kueleza baadhi ya aliyoyasoma. | Anasoma sehemu za makala. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Kuandika Insha: Insha za Wasifu**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu ili kuibainisha<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia sifa zake<br>c) kufurahia uandishi wa insha za wasifu kwa kueleza sifa za mtu, kitu, mnyama au mahali. | Mwanafunzi:<br>• akuze hamu ya ujifunzaji kwa kutazama nakala za insha ya wasifu kwenye chapa au kwenye tarakilishi<br>• atambue vipengele muhimu vya kimuundo (*k.v. kichwa, mwili, hitimisho*) katika uandishi wa insha ya wasifu<br>• akuze umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kujadili na wenzake kuhusu mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu<br>• aandike kwenye kitabu chake au kwenye tarakilishi insha ya wasifu isiyopungua maneno 200 kwa kuzingatia msamiati na ujumbe unaohusu suala lengwa. Pia azingatie ujumbe, tahajia, anwani, muundo na mtindo<br>• awasomee wenzake insha aliyoiandika. | Insha ya wasifu ina sifa gani? |



Not for Sale

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma nakala mbalimbali za insha ya wasifu.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi katika utungaji wa insha ya wasifu.<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapotunga insha ya wasifu.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiria kuhusu hoja za insha atakayoandika.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Stadi za maisha – anapotunga insha ya wasifu<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegea mada ya insha.</td><td>Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – anapoheshimu maoni ya wenzake wanapojadili.<br>• Uwajibikaji – anapoandika insha na kuikamilisha kwa wakati.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<br>• Social Studies – somo hili linafunza kuhusu watu mashuhuri katika kijamii.<br>• English – somo hili hushughulikia uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha.</td><td>Mapendekezo ya Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Mwanafunzi anakuwa kielelezo bora kwa wenzake katika jamii katika uandishi. Aidha, atajifunza kutokana na wasifu unaotolewa na wanajamii kama vile kuhusu watu mashuhuri.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu. | Anatambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu kwa urahisi. | Anatambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu. | Anatambua baadhi ya vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu. | Anatambua baadhi ya vipengele vya kimuundo vya baadhi ya insha za wasifu. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu kwa ufasaha. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Umoja na Wingi wa Nomino: Ngeli ya I-I**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya I-I katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya I-I katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-I (*k.v. chumvi, miwani na sukari, chai, kahawa, mirathi, asali, sharubati*) kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-I katika sentensi<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-I katika kifungu kifupi<br>• aandike nomino katika ngeli ya I-I katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya I-I kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya I-I kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya I-I ? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi. | | | | |

<table>
<tr><td colspan="2">

- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga maneno.
- Ujuzi wa kidijitali – kutumia tarakilishi kutambua nomino na ngeli zake.

</td></tr>
<tr><td>

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii – kufanya kazi kwa vikundi.
- Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani.

</td><td>

**Uhusiano na Maadili**

- Uwajibikaji – kutunza vipakatalishi anavyotumia.
- Uzalendo – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi.

</td></tr>
<tr><td>

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia nomino.

</td><td>

**Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**

- Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha katika shughuli za kijamii na pia kujifunza kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii ili kuimarisha mawasiliano.

</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino katika ngeli ya I-I katika matini mbalimbali. | Anatambua nomino katika ngeli ya I-I katika matini mbalimbali kwa urahisi. | Anatambua nomino katika ngeli ya I-I matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya nomino katika ngeli ya I-I katika matini mbalimbali. | Anatatizika kutambua nomino katika ngeli ya I-I katika matini. |
| Kuandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi. | Anaandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi kwa urahisi. | Anaandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi. | Anaandika baadhi ya nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi. | Ana changamoto kuandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi. |
| Kuandika umoja na | Anaandika kwa urahisi | Anaandika umoja na | Anaandika umoja na | Ana changamoto |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I | umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I. | wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I. | wingi wa baadhi ya mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I. | kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.2 Umoja na Wingi wa Sentensi: Ngeli ya I-I (Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya I-I katika mawasiliano | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya I-I katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya I-I katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya I-I kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya I-I akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya I-I kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | Je, nomino za ngeli ya I-I huchukua viambishi gani katika sentensi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi
- Kujiamini – mwanafunzi anapotumia viambishi vya ngeli ya I-I ipasavyo katika sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – kutumia tarakilishi kutambua nomino na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kufanya kazi kwa vikundi. | • Uwajibikaji – kutunza vipakatalishi anavyotumia.<br>• Uzalendo – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi. |



Not for Sale

| | |
|---|---|
| • Stadi za Maisha – kujifanyia kazi darasani. | |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza ngeli. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. Vilevile, anajifunza kutokana na matumizi ya lugha katika shughuli za kijamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi. | Anatambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi kwa urahisi. | Anatambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye baadhi ya sentensi. |
| Kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi kwa urahisi. | Anatunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia baadhi ya nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi. |

| 7.0 MAJANGA NA JINSI YA KUYAZUIA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Nahau: Nahau za Kazi na Ushirikiano**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nahau za kazi na ushirikiano katika matini mbalimbali<br>b) kujadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano ili kuzitofautisha<br>c) kutumia nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano<br>d) kuthamini matumizi ya nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nahau za kazi na ushirikiano (*k.v. chapa kazi, kunja jamvi, changa bia, sema kwa sauti moja, fanya itifaki*) katika chati, michoro, picha, vikapu maneno, mti maneno, chati, kamusi na katika vyombo vya kidijitali<br>• ashiriki katika kujadili na wenzake maana za nahau za kazi na ushirikiano kwa kutoa mifano<br>• aambatanishe nahau na maana yake<br>• atumie nahau za kazi na ushirikiano katika sentensi akiwa pekee au kwa kushirikiana na wenzake<br>• asakure mtandaoni ili kupata nahau zaidi za kazi na ushirikiano na maana zake na kuziandika | Je, ni nahau zipi zinazohimiza watu kufanya mambo mbalimbali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • awasomee wenzake nahau alizozipata ili kuelimishana. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapotafuta maana za nahau na kuzitumia kwa ufasaha katika mawasiliano.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiria kuhusu maana za nahau na matumizi yake.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – wanafunzi wanaposhiriki katika majadiliano katika vikundi.<br>• Stadi za Maisha – kutumia nahau kuimarisha mawasiliano. | • Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi pamoja katika vikundi.<br>• Heshima – wanapoheshimiana katika kazi ya vikundi. |
| **Uhusianona Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages- masomo haya hushughulikia nahau. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na katika jamii kuhusu umuhimu wa kutumia nahau kwa uboreshaji wa lugha.<br>• Ajifunze kutoka kwa wenzake kuhusu nahau za kazi na ushirikiano wanazozijua na jinsi zinavyoweza kutumika katika mawasliano. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nahau za kazi na ushirikiano. | Anatambua nahau za kazi na ushirikiano kwa urahisi. | Anatambua nahau za kazi na ushirikiano. | Anatambua baadhi ya nahau za kazi na ushirikiano. | Anatatizika kutambua nahau za kazi na ushirikiano. |
| Kujadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano. | Anajadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano kwa wepesi. | Anajadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano. | Anajadili maana ya baadhi ya nahau kazi na ushirikiano. | Ana changamoto kujadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano. |
| Kutumia nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia kwa ufasaha nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Anatatizika kutumia nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini**<br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>b) kuchagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>c) kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa<br>d) kufurahia usomaji wa matini za aina mbalimbali ili kujenga utamaduni wa kusoma. | Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za matini (*k.v. vitabu, magazeti, na majarida)* kwenye tarakilishi au kadi za katalogi<br>• ajichagulie matini atakayoisoma<br>• asome matini kimyakimya ili kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha<br>• asimulie ujumbe kutokana na matini alizosoma kwa wenzake<br>• ajadiliane na wenzake matini alizosoma ili kuchochea hamu ya usomaji wa mapana miongoni mwao. | 1. Unapenda kusoma matini ya aina gani?<br>2. Ni vipi unavyoweza kupata matini ya kusoma?<br>3. Kusoma aina mbalimbali za matini kuna umuhimu gani? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – anaposoma na kusimulia ujumbe aliosoma kutokna na matini za aina mbalimbali.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – anaposoma matini mbalimbali kuhusu majanga na jinsi ya kuyazuia ili kupata ujumbe.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Stadi za maisha – anapojenga uwezo wa kuyakabili | • Heshima – anaposhirikiana na wengine na kuzingatia |

| | |
|---|---|
| majanga. | maoni katika mijadala.<br>• Uwajibikaji – anapoazima, kutunza na kurudisha vitabu maktabani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• Social Studies - somo hili linapofundisha jinsi ya kuyadhibiti majanga.<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia kusoma kwa mapana. | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi ashiriki katika utunzaji wa vitabu katika maktaba ya shule au iliyo karibu naye nyumbani.<br>• Ajifunze kutoka kwa mkutubi kuhusu matini mbalimbali anazoweza kufaidika nazo na kuzisoma. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anatambua kwa wepesi matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anatambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anatambua baadhi ya matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anatatizika kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. |
| Kuchagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anachagua kwa makini matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anachagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Anachagua baadhi ya matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. | Ana changamoto kuchagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba. |
| Kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa. | Anasoma kwa ufasaha matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa. | Anasoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa. | Anasoma baadhi ya matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa. | Anasoma kwa shida matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Kuandika Insha:** Insha za Maelezo (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maudhui ya insha ya maelezo ili kukuza ubunifu.<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia mada, mtiririko, sarufi, muundo na mtindo ufaao<br>c) kuchangamkia utungaji wa insha za maelezo ili kukuza hali ya kujiamini. | Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya insha za maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi (*k.v. maelezo kuhusu kuzuia mmomonyoko wa udongo, mafuriko, mitetemeko ya ardhi, mkurupuko wa magonjwa kama vile kipindupindu*)<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada na vidokezo vya insha insha atakayoiandika<br>• aandike insha ya maelezo isiyopungua maneno 200 akizingatia kategoria za maneno kama vile aina mbalimbali za viwakilishi ifaavyo ili kuuwasilisha ujumbe lengwa, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya | Unazingatia nini unapoandika insha ya maelezo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali<br>• atunge insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisoma na kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**:

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.
- Kujiamini – anapofanikiwa kutunga insha ya maelezo.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**:<br>• Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Stadi za maisha – anapotunga insha na kujieleza kwa kurejelea mazingira anamoishi. | **Uhusiano na Maadili**:<br>• Heshima - hasa katika shughuli za vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**:<br>• Social Studies – masomo haya yanashughulikia jinsi ya kuyadhibiti majanga.<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia uandishi wa insha. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na katika huduma za kijamii kuhusu umuhimu wa uandishi mzuri wa maelezo. Aidha, kujifunza kutokana na maelezo yanayotolea katika shughuli za kijamii. |



Not for Sale

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuibua maudhui ya insha ya maelezo ili kuzingatia mada. | Anaibua maudhui ya insha ya maelezo kwa wepesi na kuzingatia mada. | Anaibua maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia mada. | Anaibua baadhi ya maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia mada. | Anaibua baadhi ya maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia baadhi ya mada. |
| Kuandika insha ya maelezo inayozingatia aina mbalimbali za viwakilishi kwa ufasaha kujenga picha dhahiri, yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Anaandika insha ya maelezo inayozingatia aina mbalimbali za viwakilishi kwa ufasaha kujenga picha dhahiri, akizingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Anaandika insha ya maelezo inayozingatia aina mbalimbali za viwakilishi kwa ufasaha kujenga picha dhahiri, akizingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo inayozingatia aina mbalimbali za viwakilishi kwa uchache, akizingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo bila kutumia vizuri aina mbalimbali za viwakilishi na kanuni za lugha. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Umoja na Wingi wa Nomino na Sentensi: Ngeli ya PA-KU-MU (Kipindi 1)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya PA-KU-MU ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi<br>c) kuandika sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya PA-KU-MU kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno (*k.v: huku, humu, hapa, hapo, huko, humo, pale, kule, mle*)<br>• aandike nomino katika ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya PA-KU-MU kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• abadilishe sentensi zenye nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya PA-KU-MU akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya PA-KU- | Nonimo za ngeli ya PA-KU-MU ni gani? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | MU kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – anapotumia tarakilishi kutambua nomino na ngeli ya PA-KU-MU

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji – kutunza vipakatalishi anavyotumia.<br>• Uzalendo – kufanya kazi na wengine kwenye vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hufunza dhana ya nomino. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika huduma za kijamii huku akijifunza kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino katika ngeli ya PA-KU-MU. | Mwanafunzi anatambua nomino katika ngeli ya PA-KU-MU kwa wepesi. | Mwanafunzi anatambua nomino katika ngeli ya PA-KU-MU. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino katika ngeli ya PA-KU-MU. | Mwanafunzi anajaribu kutambua nomino katika ngeli ya PA-KU-MU. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika kwa urahisi nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika baadhi za nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anatatizika kuandika nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. |
| Kuandika sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika kwa wepesi sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anaandika baadhi ya sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. | Mwanafunzi anajaribu kuandika sentensi akitumia nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi. |

| 8.0 WANYAMA WA MAJINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1 Visawe vya Maneno Zaidi ya Matatu**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno<br>b) kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano<br>c) kuthamini matumizi ya maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa (*k.v. mwizi-luja, mkupuzi, pwagu, pwaguzi, mkwepuzi; hongo, rushwa, chai, kadhongo, mvugulio; pesa - njenje, ngwenje, fedha, hela; lengo - dhamira, nia, azma, kusudi; maskini, mlalahoi, fukara, mkata, fakiri)* kwa kutumia kapu la maneno, kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi, n.k.<br>• eleze maana ya maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa akiwa peke yake au kwa kujadiliana na wenzake katika kikundi<br>• ambatanishe maneno zaidi ya matatu yaliyo na maana sawa katika kapu la maneno, mti wa maneno, ubao, chati, vyombo vya kidijitali, kadi za maneno n.k.<br>• ahusishe visawe na vifaa halisi, picha, michoro kwenye chati, | Unajua maneno gani ya Kiswahili yaliyo na maana sawa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kitabu au katika vyombo vya kidijitali<br>• ashiriki kujadili visawe mbalimbali katika vikundi au wanafunzi wawiliwawili<br>• atumie kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwnafunzi anapofikiria kuhusu visawe mwafaka.
- Ujuzi wa kidigitali - anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua visawe.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii - kwa kufanya kazi katika vikundi.<br>• Stadi za Maisha - katika kujieleza kwa visawe mbalimbali. | • Sentensi zitakazorejelewa zijumuishe maadili mbalimbali k.v. umoja, uzalendo, uwajibikaji na upendo. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English – somo hili linafunza dhana ya visawe. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awe kielelezo kwa wanajamii katika kutumia lugha mwafaka na maneno tofauti kujieleza huku akijifunza kutokana na matumizi ya lugha anayopata kutoka kwa jamii. |



Not for Sale

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno. | Anatambua kwa urahisi maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno. | Anatambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno. | Anatambua baadhi ya maneno yenye maana sawa katika kundi la maneno. | Anatatizika kutambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno. |
| Kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano. | Anatumia visawe ifaavyo na kwa wepesi katika mawasiliano. | Anatumia visawe ifaavyo katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya visawe ifaavyo katika mawasiliano. | Ana changamoto kutumia visawe katika mawasiliano. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Mchezo wa Kuigiza**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili sifa za mchezo wa kuigiza ili kuzibainisha<br>b) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa<br>c) kuonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari<br>d) kuonea fahari nafasi ya mchezo wa kuigiza katika jamii. | Mwanafunzi:<br>• aeleze maana ya mchezo wa kuigiza akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• ajadili na wenzake sifa za mchezo wa kuigiza (*k.v. huwa na wahusika, kuna mazungumzo, maelekezo n.k.*)<br>• asome mchezo wa kuigiza akizingatia wahusika, maelekezo na ujumbe<br>• atambue msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza (*k.v. kiboko, samaki, mamba, chura, kasa*)<br>• ashiriki katika majadiliano kuhusu msamiati uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza<br>• ajibu maswali kutokana | 1. Je, mchezo wa kuigiza una sifa gani?<br>2. Umewahi kushiriki katika mchezo gani wa kuigiza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na mchezo aliousoma<br>• atoe muhtasari wa ujumbe ulio katika mchezo wa kuigiza<br>• atazame mchezo mfupi wa kuigiza shuleni au kwenye vifaa vya kidijitali<br>• ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza<br>• asaidiwe na mzazi au mlezi wake kusakura na kusoma mchezo wa kuigiza kwenye mtandao<br>• awaeleze wenzake darasani ujumbe alioupata kutoka kwa mchezo aliousoma mtandaoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mchakato wa ujifunzaji.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiri kuhusu ujumbe uliomo kwenye mchezo wa kuigiza.
- Kujiamini – mwanafunzi anapong’amua ujumbe uliomo kwenye mchezo wa kuigiza.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Masuala mtambuko anuwai yanayojitokeza katika mchezo wa kuigiza (*k.m. utunzaji wa wanyama wa porini, masuala ya afya, utunzaji wa misitu*) | • Heshima – mwanafunzi anapoheshimu uigizaji wa wenzake.<br>• Umoja – wanaposhrikiana kuigiza mchezo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia mchezo wa kuigiza. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wengine kuhusu umuhimu wa mchezo wa kuigiza katika mawasiliano.<br>• Ajifunze uigizaji kutokana na maigizo kwenye shughuli za kijamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili sifa za mchezo wa kuigiza ipasavyo. | Anajadili sifa za mchezo wa kuigiza ipasavyo na kwa ufasaha. | Anajadili sifa za mchezo wa kuigiza ipasavyo. | Anajadili baadhi ya sifa za mchezo wa kuigiza ipasavyo. | Ana changamoto kujadili sifa za mchezo wa kuigiza. |
| Kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa. | Anasoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha na wepesi kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa. | Anasoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa | Anasoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia baadhi ya ujumbe na msamiati wa suala lengwa. | Anasoma mchezo mfupi wa kuigiza bila kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa. |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari. | Anaonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari kwa ukakamavu. | Anaonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari. | Anaonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu baadhi ya maswali na kutoa muhtasari. | Ana changamoto kujibu maswali ya mchezo wa kuigiza na kutoa muhtasari. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Kuandika Insha:**<br><br>Insha za Masimulizi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze,<br>a) kujadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri katika uandishi wa insha ya masimulizi. | Mwanafunzi:<br>• ajadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili muundo wa insha ya masimulizi<br>• aonyeshe ubunifu kwa kuandika insha isiyopungua maneno 200 inayosimulia tukio linalohusiana na wanyama wa porini akizingatia nomino na vivumishi mbalimbali, mnyambuliko wa vitenzi, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka, lugha ya kiubunifu na urefu unaotarajiwa<br>• akuze ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya masimuizi katika vifaa vya kidijitali na | Ni nini unachoweza kufanya ili uwe mwandishi bora wa insha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimuizi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya masimuizi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegea mada ya insha. | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – hasa katika shughuli za vikundi.<br>• Insha za wasifu zaweza kulenga watu ambao wanajulikana kwa uaminifu, uwajibikaji, wenye mapenzi na wazalendo. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English na Indigenous Language – masomo haya yanashughulikia uandishi wa insha za masimulizi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na katika jamii kuhusu umuhimu wa uandishi bora wa masimulizi huku akijifunza kutokana na masimulizi mbalimbali katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi. | Anajadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi kwa ubunifu. | Anajadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi. | Anajadili mtiririko wa baadhi ya hoja katika insha ya masimulizi. | Anajadili mtiririko wa baadhi ya hoja katika baadhi ya insha za masimulizi. |
| Kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu kwa ufasaha na urefu uliopendekezwa. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha lugha, mpangilio mzuri wa mawazo, lugha ya kiubunifu na urefu ufao. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |



Not for Sale

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi: Kauli ya Kutendeana, Kutendesha, Kutendua**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo katika sentensi<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha na kutendua katika chati, jedwali, kapu la maneno, mti wa maneno, ubao na vyombo vya kidijitali<br>• anyambue vitenzi katika hali lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawiliwawili au katika vikundi<br>• atumie vitenzi katika hali lengwa kwenye sentensi<br>• ashirikiane na wenzake kujaza mapengo katika jedwali la mnyambuliko we vitenzi kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi<br>• aandike sentensi upya kwa kutumia vitenzi katika hali mbalimbali. | Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano –- kufanya kazi wakiwa wawiliwawili na katika vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi ananyambua vitenzi katika hali mbalimbali.
- Kujiamini – anapotoa majibu na kushiriki katika shughuli mbalimbali.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii: kufanya kazi pamoja<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutokana na sentensi zilizotungwa. | • Maadili mbalimbali k.v. upendo, umoja, heshima, uzalendo n.k. kutokana na sentensi zilizotungwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English – somo hili hushughulikia suala la mnyambuliko wa vitenzi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awe kielelezo cha matumizi ya lugha ifaavyo katika kuwasilisha ujumbe katika huduma za kijamii. Aidha, ajifunze kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini. | Anatambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini kwa urahisi. | Anatambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini. | Anatambua baadhi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini. | Anatambua baadhi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika baadhi ya matini. |
| Kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo anapowasiliana. | Anatumia kwa urahisi vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo anapowasiliana. | Anatumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo anapowasiliana. | Anatumia baadhi ya vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo anapowasiliana. | Ana changamoto kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo anapowasiliana. |



Not for Sale

| 9.0 AFYA YA AKILI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo ya Kimuktadha:**<br><br>**Mazungumzo katika miktadha rasmi na isiyo rasmi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miktadha rasmi na isiyo rasmi katika mawasiliano ili kuitofautisha<br>b) kutumia lugha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi ili kufanikisha mawasiliano.<br>c) Kuchangamkia matumizi ya lugha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi kuimarisha maadili yafaayo. | Mwanafunzi:<br>• atambue miktadha mbalimbali kunakotumiwa lugha rasmi na isiyo rasmi *(k.v. ofisini, hospitalini, nyumbani, sokoni)*<br>• asikilize mazungumzo rasmi na yasiyo rasmi kwa kutazama maigizo kwenye vyombo vya kidijitali *(k.v. video, rununu, runinga, tarakilishi)*<br>• ashiriki katika maigizo ya mazungumzo ya miktadha rasmi na yasiyo rasmi akishirikiana na wenzake<br>• ashiriki katika mazungumzo rasmi nje ya darasa k.m. akiwa kwenye gwaride, majilisini n.k na yale yasiyo rasmi kama vile uwanjani, kwenye bweni, katika safari ya kwenda nyumbani kutoka shuleni | 1. Ni wapi katika shughuli zetu za kila siku tunaitumia lugha rasmi na isiyo rasmi?<br><br>2. Ni nini kinachofanya mazungumzo yawe rasmi au yasiyo rasmi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • atambue, nidhamu ya lugha inayozingatiwa katika mazingira rasmi (*k.m lugha ya heshima na adabu anapowasiliana*). | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – kupitia kwa kushiriki kazi ya vikundi.
- Ubunifu – anapobuni na kushiriki katika mazungumzo.
- Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza na kutazama mazungumzo.

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**

- Mazungumzo yahusishe masuala mtambuko k.v umuhimu wa usingizi wa kutosha, lishe bora.

**Uhusiano na Maadili**

- Uwajibikaji – katika kutunza vifaa vya kidijitali.
- Heshima na ushirikiano – katika uigizaji na kushiriki katika mazungumzo.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia mazungumzo katika miktadha rasmi na isiyo.

**Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**

- Mwanafunzi awe kielelezo kwa wengine katika kutumia lugha kwa heshima na ufasaha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.
- Ajifunze lugha ya heshima inayotumika katika jamii katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua miktadha rasmi na isiyo rasmi katika mawasiliano. | Anatambua kwa urahisi miktadha rasmi na isiyo rasmi ya mawasiliano. | Anatambua miktadha rasmi na isiyo rasmi ya mawasiliano. | Anatambua baadhi ya miktadha rasmi na isiyo rasmi ya mawasiliano. | Ana changamoto kutambua miktadha rasmi na isiyo rasmi katika mawasiliano. |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuitumia lugha ipasavyo katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. | Anaitumia lugha ipasavyo na kwa ukakamavu katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. | Anaitumia lugha ipasavyo katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. | Anaitumia lugha ipasavyo katika baadhi ya miktadha rasmi na isiyo rasmi. | Anatatizika kuitumia lugha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi kuwasiliana. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina mbalimbali za matini ili kuchagua inayomvutia<br>b) kusoma matini aliyochagua ili kufaidika na ujumbe na lugha iliyotumiwa<br>c) kufurahia usomaji wa aina mbalimbali za matini ili kupanua mawazo yake | Mwanafunzi:<br>• atambue matini zinazomvutia maktabani na mtandaoni<br>• asome matini alizochagua ili kufaidi ujumbe na lugha iliyotumiwa<br>• awatolee wenzake muhtasari wa kile alichosoma kwenye matini ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha<br>• ajadiliane na wenzake matini ambazo wamesoma kwa kuzingatia ukuzaji wa msamiati. | 1. Ni habari zipi unazopenda kusoma kwenye matini?<br>2. Unazingatia nini unapochagua matini za kusoma? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposimulia na kujadiliana na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi na mtandao kupata matini za kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojichagulia matini na kuzisoma.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Masuala mtambuko mbalimbali katika matini za kusoma (*k.v. Afya ya akili, afya ya mwili, msongo wa mawazo)* | • Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza matini anazosoma.<br>• Heshima – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu alichosoma. |

| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
|---|---|
| • English – somo hili hushughulikia kusoma kwa mapana. | • Kuwa kielelezo cha utamaduni wa kusoma shuleni na nyumbani<br>• Maarifa anayopata mwanafunzi kutokana na usomaji wake anayatumia shuleni na nyumbani kuifaidi jamii.<br>• Ajifunze kutokana na jamii kuhusu matini mbalimbali zinazoweza kumfaidi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua matini za aina mbalimbali za kusoma na kuchagua zinazomvutia. | Anatambua kwa urahisi matini za aina mbalimbali za kusoma na kuchagua zinazomvutia. | Anatambua matini za aina mbalimbali za kusoma na kuchagua zinazomvutia. | Anatambua matini chache tu za kusoma na kuchagua zinazomvutia. | Atatizika kutambua matini za aina mbalimbali za kusoma. |
| Kusoma matini alizochagua na kueleza kwa ufasaha ujumbe alioupata. | Anasoma matini alizochagua na kueleza kwa ufasaha na wepesi ujumbe alioupata. | Anasoma matini alizochagua na kueleza kwa ufasaha ujumbe alioupata. | Anasoma matini alizochagua na kueleza ujumbe alioupata | Anatatizika kusoma matini alizochagua na pia ana changamoto kueleza ujumbe alioupata. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Kuandika Insha:** Insha za Maelezo<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze,<br>a) kueleza maudhui ya insha ya maelezo kwa kuzingatia mada<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo ili kufanikisha mawasiliano<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wenye mapambo ya lugha. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake kukuza uwazaji kina na utatuzi wa matatizo kwa kueleza maudhui kutokana na mada ya insha ya maelezo<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo<br>• aandike insha ya maelezo akitumia vivumishi na vielezi vifaavyo kutoa picha dhahiri kuhusu anachokielezea. Pia akizingatie anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na lugha ya kiubunifu inaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali<br>• akuze umilisi wa ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na | Je, ni mada gani inayoweza kuandikiwa insha za maelezo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisoma na kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano –wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii – kutokana na kufanya kazi pamoja katika vikundi.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegea mada ya insha. | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – hasa katika shughuli za vikundi<br>• Upendo – wanafunzi wanapofanya kazi pamoja. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia mada kuandika. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na katika jamii kuhusu umuhimu wa uandishi mzuri katika mawasiliano. Pia, kujifunza kutokana na maelezo anayopata katika shughuli za huduma kwa jamii. |

**igezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maudhui ya insha ya maelezo ili kuzingatia mada. | Anaeleza maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia mada kwa ubunifu. | Anaeleza maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia mada. | Anaeleza baadhi ya maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia mada. | Anaeleza baadhi ya maudhui ya insha ya maelezo na kuzingatia baadhi ya mada. |
| Kuandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Anaandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya maelezo bila kujenga picha dhahiri ya anachoandikia. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Vinyume vya Vivumishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vivumishi katika matini<br>b) kutunga sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi<br>c) kuchangamkia matumizi ya vinyume vya vivumishi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi:<br>• atambue vinyume vya vivumishi (*k.v. zuri- baya, kali-butu, refu-fupi*) katika chati, kadi za maneno, kapu la maneno, mti wa maneno au vifaa vya kidijitali<br>• ashirikiane na wengine kutafuta vinyume vya vivumishi kwa kurejelea orodha ya vivumishi alivyopewa<br>• atalii mazingira yake na kuunda orodha ya vinyume vya vivumishi<br>• atunge sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. | Je, ni vivumishi vipi unavyoweza kutambua vinyume vyake? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – kupitia kwa kushiriki kazi ya vikundi.
- Ubunifu – anapotunga sentensi sahihi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Elimu ya mazingira – Mwanafunzi anapanua mawazo kuhusu mazingira yake anapotambua vinyume vya | • Uwajibikaji – katika kutunza vifaa vya kidijitali.<br>• Heshima – katika shughuli za vikundi. |

| | |
|---|---|
| vivumishi kutoka kwenye mazingira yake. | |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English – somo hili hushughulikia dhana ya vinyume. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi awe kielelezo kwa wengine katika kutumia lugha kwa ufasaha anaposhiriki katika shughuli za huduma kwa jamii. Aidha, atajifunza matumizi ya vinyume vinavyotumika katika muktadha wa huduma kwa jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vinyume vya vivumishi katika matini. | Anatambua vinyume vya vivumishi katika matini kwa urahisi. | Anatambua vinyume vya vivumishi katika matini. | Anatambua baadhi ya vinyume vya vivumishi katika matini. | Anatambua baadhi ya vinyume vya vivumishi katika baadhi ya matini. |
| Kutunga sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi. | Anatunga sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi kwa urahisi. | Anatunga sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi. | Anatunga baadhi ya sentensi kwa kutumia vinyume vya vivumishi. | Anatunga baadhi ya sentensi kwa kutumia baadhi ya vinyume vya vivumishi. |



Not for Sale

| 10.0 KUKABILIANA NA UGAIDI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Ulinganisho wa Moja kwa Moja** (Sitiari za Tabia)<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili dhana ya sitiari ili kuitofautisha na dhana zingine za lugha<br>b) kutambua sitiari za tabia katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>c) kutumia sitiari za tabia kwa usahihi katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kufurahia matumizi ya sitiari katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi:<br>• ajadili na mwenzake au katika kikundi maana ya sitiari<br>• atambue sitiari za tabia (*k.v. yeye ni sungura, yeye ni fisi, yeye ni kasuku, mimi ni kobe safarini*) katika vitabu, matini, chati na vyombo vya kidijitali akiwa peke yake au katika kikundi<br>• atoe mifano ya sitiari za tabia akisaidiana na mwenzake<br>• aeleze maana ya sitiari mbalimbali<br>• atumie sitiari katika sentensi akiwa peke yake au katika vikundi.<br>• akisaidiwa na mzazi au mlezi, atunge sentensi mbalimbali akitumia sitiari za tabia<br>• awasilishe sentensi zake darasani ili wenzake wazitolee maoni. | Ni maneno gani unayoweza kutumia kulinganisha kitu na kingine kwa njia ya moja kwa moja? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano –mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya vikundi.</li><li>Hamu ya ujifunzaji – kutokana na kutambua sitiari katika matini.</li><li>Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua sitiari.</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<ul><li>Stadi za maisha hasa katika kuimarisha mawasiliano.</li></ul></td><td>Uhusiano na Maadili<ul><li>Heshima – anapoheshimu maoni ya wenzake katika vikundi.</li><li>Umoja – anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.</li></ul></td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<ul><li>English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia dhana ya sitiari.</li></ul></td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<ul><li>Kuwa kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha shuleni na katika jamii. Pia, kujifunza matumizi ya lugha anapotangamana na wanajamii.</li></ul></td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili dhana ya sitiari ipasavyo. | Anajadili dhana ya sitiari ipasavyo na kutoa mifano. | Anajadili dhana ya sitiari ipasavyo. | Anajaribu kujadili dhana ya sitiari | Anatatizika kujadili dhana ya sitiari. |
| Kutambua sitiari za tabia katika matini mbalimbali | Anatambua kwa weledi sitiari za tabia katika matini mbalimbali. | Anatambua sitiari za tabia katika matini mbalimbali. | Anatambua baadhi ya sitiari za tabia katika matini mbalimbali. | Ana changamoto kutambua sitiari za tabia katika matini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia sitiari za tabia kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia sitiari za tabia kwa usahihi na ufasaha katika sentensi. | Anatumia sitiari za tabia kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya sitiari za tabia kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya sitiari za tabia katika sentensi bila usahihi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini za Kidijitali**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma ili kuimarisha umilisi wake wa kutumia tarakilishi<br>b) kuonyesha uelewa wa hatua za kiusalama kwa kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma kutumia vyombo vya kidijitali<br>c) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | Mwanafunzi:<br>• atambue mambo ya kuzingatia anaposoma matini zilizohifadhiwa katika kifaa cha kidijitali (*k.v. kutofuta kazi za wengine zilizohifadhiwa katika vifaa vya kidijitali*) akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• atambue mambo ya kuzingatia anaposoma matini za mtandaoni *(k.v. kufungua mitandao ifaayo, kutowasiliana na watu usiowajua, kutofichua nywila yako kwa wengine*)<br>• atambue jina la faili lengwa kwenye tarakilishi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga<br>• atambue mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake<br>• atambue umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao<br>• atafute maana za maneno mapya kwenye kamusi mtandaoni | 1. Unakumbuka habari gani uliyoisoma mtandaoni?<br>2. Ni hatua gani za kiusalama unazozingatia unapotafuta habari mtandaoni? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • asimulie wenzake habari alizosoma. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya vifaa vya kiteknolojia katika kutafuta, kusakura na kusoma.
- Hamu ya kujifunza – mwanafunzi atapata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Stadi za maisha – ujuzi wa kidijitali na usalama mitandaoni. | • Uwajibikaji – katika utunzaji wa vifaa vya kidijitali na kuzingatia mitandao salama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• Masomo yote kwa vile yanatakiwa kuzingatia ujuzi wa kidijitali. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na katika jamii kuhusu usalama mitandaoni na manufaa ya ujuzi wa kidijitali katika kuimarisha usomaji na kupata maarifa yanayohusu nyanja mbalimbali. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi. | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi na wepesi. | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi. | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma. | Ana changamoto kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma. |
| Kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. | Anasakura kwenye tovuti salama kwa wepesi ili kupata vifungu vya kusoma. | Anasakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. | Anasakura kwenye tovuti salama ili kupata baadhi ya vifungu vya kusoma. | Anatatizika kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Kuandika: Insha za Masimulizi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kueleza maudhui ya insha ya masimulizi ili kuandika ifaavyo<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada na vidokezo vya insha ili kuvitumia katika kuandika insha yake<br>• ashirikiane na wenzake katika kundi kuelezea maudhui atakayotumia kuandikia insha ya masimulizi<br>• aandike insha ya masimulizi (*k.v. kuhusu ugaidi, uhalifu, ajali, safari n.k*) isiyopungua maneno 200 akizingatia mada, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka, lugha ya kiubunifu na urefu unaotarajiwa. Pia azingatie aina mbalimbali za maneno, mnyambuliko wa vitenzi, na | Insha ya masimulizi ina sifa gani? |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | nyakati ili kejenga picha dhahiri ya anachokiandikia daftarini.<br>• aandike insha ya masimulizi katika vifaa vya kidijitali na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya mawasiliano.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika insha ya masiliano.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – kutokana na kufanya kazi pamoja katika vikundi.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea mada ya insha. | • Heshima – hasa katika shughuli za vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• English na Indigenous Language – masomo haya yanafunza uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na katika jamii kuhusu umuhimu wa uandishi bora wa masimulizi katika mawasiliano. Aidha, atajifunza kutokana na masimulizi yanayotolewa kuhusu matukio mbalimbali katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maudhui ya insha ya masimulizi. | Anaeleza maudhui ya insha ya masimulizi kwa ubunifu. | Anaeleza maudhui ya insha ya masimulizi. | Anaeleza baadhi ya maudhui ya insha ya masimulizi. | Ana changamoto kueleza maudhui ya insha ya masimulizi. |
| Kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu na urefu ufaao. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha lugha, mpangilio mzuri wa mawazo. | Anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Matumizi ya Lugha:** Hali ya Masharti<br>-nge<br>-ngali<br>-ki<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya hali ya masharti kwenye kitenzi<br>b) kutumia vitenzi katika hali ya masharti kwenye sentensi<br>c) kufurahia matumizi ya hali ya masharti katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya hali ya masharti (**nge, ngali, ki**) kwenye vitenzi katika chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali<br>• atumie vitenzi vya hali ya masharti katika sentensi<br>• ashiriki na wenzake katika mazoezi ya kutumia hali ya masharti kwa kuandika daftarini au kupiga chapa kwenye tarakilishi/kipakatalishi<br>• ashirikiane na wenzake katika vikundi kubadilisha sentensi kutoka hali moja hadi nyingine<br>• atunge sentensi katika hali ya mazoea na hali ya masharti mtandaoni na kuwatumia wenzake waweze kuzisoma na kutathmini usahihi wake. | Je, unaelezea vipi iwapo hukulifanya jambo fulani kutokana na ukosefu wa kitu, jambo au mtu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika shughuli za vikundi darasani na mtandaoni.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kutunga sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kipakatalishi au tarakilishi kutunga sentensi na vile vile kuzisambaza mtandaoni.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
| --- | --- |
| • Stadi za maisha – kujitambua na kujithamini anapotunga sentensi na kuzitumia kujieleza. | • Heshima – anapojifunza kuthamini maoni ya wengine.<br>• Upendo – anaposhirikiana na wengine katika kazi za vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English – somo hili hushughulikia hali ya masharti. | • Mwanafunzi anapokuwa kielelelzo kwa wenzake shuleni na jamiikatika kutumia Kiswahili kwa kuzingatia kanuni za kisarufi. Aidha, anapojifunza matumizi ya lugha kutokana na kutangamana na jamii katika shughuli za huduma kwa jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| Kutambua viambishi vya hali ya masharti kwenye kitenzi. | Anatambua viambishi vya hali ya masharti kwenye kitenzi kwa urahisi. | Anatambua viambishi vya hali ya masharti kwenye kitenzi. | Anatambua baadhi ya viambishi vya hali ya masharti kwenye kitenzi. | Anatambua baadhi ya viambishi vya hali ya masharti kwenye baadhi ya kitenzi. |
| Kutumia vitenzi katika hali ya masharti kwenye sentensi. | Anatumia vitenzi katika hali ya masharti kwenye sentensi kwa usahihi na wepesi. | Anatumia vitenzi katika hali ya masharti kwenye sentensi. | Anatumia baadhi ya vitenzi katika hali ya masharti kwenye sentensi. | Anatumia baadhi ya vitenzi katika hali ya masharti kwenye baadhi ya sentensi. |


Not for Sale

| 11.0 USHURU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji** | **Swali Dadisi** |
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Kuzungumza na Kujieleza kwa Ufasaha: Kutoa masimulizi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada mwanafunzi aweze:<br>a) kubuni na kusimulia kisa mbele ya wenzake akizingatia mada lengwa<br>b) kutumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake<br>c) kufurahia usimulizi wa visa mbalimbali kuhusu maisha. | Mwanafunzi:<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu mada mbalimbali ambazo huweza kusimuliwa kuhusiana na mambo na hali za maisha (*k.v. hadithi za mashujaa*, *shughuli za sikukuu za kitaifa*, *usomaji wa bajeti, ulipaji wa ushuru, hekaya)*<br>• asikilize kisa cha kisimulizi kuhusu mada lengwa kutoka kwa mgeni mwalikwa, tepurekoda, video na tarakilishi ili kupata sifa za usimulizi mzuri<br>• asimulie kisa kuhusiana na mada fulani akizingatia mtiririko wa mawazo, mfuatano wa matukio, kanuni za kisarufi, kupanda na kushuka kwa sauti, ishara za uso, viziada lugha, tasfida, na wakati ili kuufanya utungo wake uvutie.<br>• ashirikishe hadhira kupitia uimbaji, kupiga makofi, kucheza, kuitikia, | Masimulizi kuhusu ushuru yana umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | n.k. ili kuupa usimulizi wake uhai zaidi na kuteka makini ya wasikilizaji<br>• aulize na kujibu maswali kutokana na visa vilivyosimuliwa darasani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ubunifu – anapotunga na kusimulia kisa kuhusu mambo mbalimbali katika jamii.
- Kujiamini – anaposimama mbele ya hadhira na kusimulia kisa.
- Ujuzi wa kidijitali – anaposikiliza masimulizi kupitia vifaa vya kielektroniki.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Elimu fedha – ujuzi wa njia mbalimbali za matumizi ya ushuru na serikali.<br>• Mshikamano wa kijamii – anaposhirikiana na wengine katika kusimulia hali mbalimbali.<br>• Hamu ya ujifunzaji – anapotafiti kuhusu kisa atakachosimulia. | • Uwajibikaji – kujitahidi kusimulia.<br>• Umoja – anaposhirikiana na wenzake kutoa masimulizi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji** |
| • English – somo hili hushughulikia suala la kutoa masimulizi.<br>• Social Studies – masomo haya yanafundisha kuhusu masuala ya kiuchumi na rasilimali. | • Anaposimulia kisa kuhusu matukio mbalimbali katika jamii na pia anapopokea maoni kutoka kwa wenzake na wanajamii kuhusu masimulizi yake. |



Not for Sale

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubuni na kusimulia kisa mbele ya wenzake akizingatia mada lengwa. | Anabuni na kusimulia kisa mbele ya wenzake kwa ukakamavu akizingatia mada lengwa. | Anabunu na kusimulia kisa mbele ya wenzake akizingatia mada lengwa. | Anabuni na kusimulia baadhi ya visa mbele ya wenzake akizingatia mada lengwa. | Ana changamoto kubuni na kusimulia kisa mbele ya wenzake akizingatia mada lengwa. |
| Kutumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake. | Anatumia kwa mvuto ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake. | Anatumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake. | Anatumia baadhi ya ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake. | Anatatizika kutumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **Kusoma kwa Ufahamu**: **Kifungu**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu<br>b) kuelezea maana ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu<br>c) kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi<br>d) kusoma kifungu ili kupata ujumbe<br>e) kujibu maswali kutokana na kifungu ili kuonyesha uelewa wa kifungu<br>f) kuchangamkia usomaji wa kifungu ili kujenga maarifa ya ufahamu. | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati unaohusu ushuru (*k.v. ushuru, ushuru wa forodhani, ushuru wa mapato, mapato, Shirika la Ukusanyaji Ushuru, mgao wa fedha, bajeti, mipakani, mshahara, afisa wa forodhani, ukwepaji wa ushuru, pesa zinazolipwa Serikali za Kaunti [k.v. za leseni, kuegesha magari, kuuza sokoni], matumizi ya mgao wa fedha)* akitumia kapu la maneno, mti wa maneno au tarakilishi<br>• atunge sentensi akitumia msamiati husika, akiwa peke yake, wawiliwawili au kikundi<br>• atazame chati kwenye tarakilishi au matini inayoonyesha matumizi ya fedha za serikali<br>• ajadili na wenzake matukio kwenye picha zinazoonyesha matumizi bora ya ushuru (*k.v. ujenzi wa barabara, hospitali, shule, usalama, n.k.)*<br>• asome kifungu kwa sauti akipishana zamu na wenzake | 1. Je, ni mambo gani yanayokuvutia unaposoma kifungu cha ufahamu?<br>2. Unafanya nini ili kujua maana ya msamiati uliotumiwa katika kifungu? |



Not for Sale

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>aulize na kujibu maswali kutokana na kifungu.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano – anaposoma kifungu au mchezo mfupi kwa sauti na kupishana nafasi na wenzake.</li><li>Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – anapojibu maswali kutokana na kifungu.</li><li>Uraia – anaposoma kuhusu ulipaji ushuru na umuhimu wake.</li><li>Kujiamini – anapoweza kujibu maswali baada ya kusoma kifungu.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<ul><li>Elimu ya fedha – anapojifunza kuhusu fedha hususan ulipaji ushuru.</li><li>Stadi za maisha – anapopata maarifa ya kujitegemea kuhusu fedha.</li></ul></td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<ul><li>Heshima – mwanafunzi anaposikiliza na kuheshimu wengine wakisoma kifungu.</li><li>Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi pamoja katika vikundi.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<ul><li>Social studies – somo hili hushughulikia suala la rasilimali katika jamii.</li></ul></td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<ul><li>Anapowahamasisha wanajamii kuhusu usomaji na pia anapojifunza usomaji kutokana na huduma za kijamii kama vile kusoma matangazo mikutanoni au shughuli zinazohusiana na maarifa ya ushuru aliyopata.</li></ul></td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu. | Anatambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu. | Anatambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu. | Anatambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu. | Anatambua msamiati lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu. |
| Kuelezea maana ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu. | Anaeleza kwa ufasaha maana ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu. | Anaeleza maana ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu. | Anaeleza maana ya baadhi ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu. | Ana changamoto kueleza maana ya msamiati lengwa uliotumiwa katika kifungu. |
| Kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia msamiati lengwa kwa usahihi na urahisi katika sentensi. | Anatumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi. | Anatumia baadhi ya msamiati lengwa kwa usahihi katika baadhi ya sentensi. |
| Kusoma kifungu ili kupata ujumbe. | Anasoma kifungu kwa ufasaha na kupata ujumbe. | Anasoma kifungu na kupata ujumbe. | Anasoma kifungu na kupata sehemu ya ujumbe. | Anasoma kifungu lakini ana changamoto kupata ujumbe. |
| Kujibu maswali kutokana na kifungu ili kuonyesha uelewa wa kifungu. | Anajibu kwa urahisi maswali kutokana na kifungu na kuonyesha uelewa wa kifungu. | Anajibu maswali kutokana na kifungu na kuonyesha uelewa wa kifungu. | Anajibu baadhi ya maswali kutokana na kifungu. | Anatatizika kujibu maswali kutokana na kifungu. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Kuandika: Barua Rasmi**<br><br>**(Vipindi 2)** | Kufikia mwisho wa mada mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maudhui ili kuandika barua rasmi inayozingatia mada<br>b) kuandika barua rasmi inayozingatia mada, hati safi, muundo na mtindo ufaaoili kuwasiliana ipasavyo<br>c) kuchangamkia utunzi wa barua rasmi katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue mada ya kuandikia barua rasmi<br>• ajadili na wenzake maudhui yafaayo kulingana na mada ya insha ya barua rasmi.<br>• aandike vidokezo vya kumwongoza<br>• ajadili na wenzake vipengele vya aya<br>• aandike barua rasmi kwa mwalimu daftarini kuomba msamaha na kuiwasilisha kila hoja katika aya yake<br>• atumie sentensi inayobeba wazo kuu mwanzoni mwa kila aya<br>• aandike kwa hati safi au kwa kutumia tarakilishi huku akizingatia kanuni zifaazo.<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano. | 1. Uandishi wa barua rasmi huzingatia vipengele gani?<br>2. Unazingatia nini ili kuunda aya nzuri? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano-anaposhirikiana na wenzake katika vikundi.<br>• Ubunifu – anapotunga na kuandika barua rasmi kwa mwalimu.<br>• Ujuzi wa kidijitali – anapoandika barua kwa kutumia tarakilishi.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegea mada ya barua rasmi.</td><td>Uhusiano na Maadili<br>• Umoja – anaposhirikiana na wengine kujadili maudhui ya barua rasmi.<br>• Heshima – anapozingatia maoni ya wengine wakati wa mijadala.<br>• Uwajibikaji – anapoandika barua rasmi kuomba msamaha.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<br>• Social Studies – somo hili hufundisha kuhusu watu mashuhuri katika jamii<br>• English – somo hili hufundisha kuhusu uandishi wa barua rasmi.</td><td>Mapendekezo ya Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Anapowashirikisha wenzake shuleni na katika jamii katika uandishi wa barua rasmi. Pia, anapojifunza kutokana na barua rasmi anazotangamana nazo katika shughuli za kijamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili maudhui ili kuandika barua rasmi inayozingatia mada. | Anajadili maudhui na kuandika barua rasmi inayozingatia mada kwa ubunifu. | Anajadili maudhui na kuandika barua rasmi inayozingatia mada. | Anajadili baadhi ya maudhui na kuandika barua rasmi inayozingatia mada. | Ana changamoto kujadili maudhui na kuandika barua rasmi inayozingatia mada. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika barua rasmi inayozingatia mada, hati safi inayosomeka na mpangilio mzuri wa aya ili kuwasiliana ipasavyo. | Anaandika barua rasmi inayozingatia mada, hati safi inayosomeka na mpangilio mzuri wa aya ili kuwasiliana ipasavyo kwa urahisi. | Anaandika barua rasmi inayozingatia mada, hati safi inayosomeka na mpangilio mzuri wa aya ili kuwasiliana ipasavyo. | Anajaribu kuandika barua rasmi inayozingatia mada kwa hati inayosomeka. | Anajaribu kuandika barua. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Ukanushaji wa Maneno: Viambishi vya hali ya masharti (nge, ngali, ki)**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya hali ya masharti katika sentensi<br>b) kukanusha viambishi vya hali ya masharti katika sentensi<br>c) kufurahia ukanushaji wa viambishi hali ya masharti katika sentensi. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya hali ya masharti (nge, ngali, ki) katika vitenzi kwa kuvipigia mistari kwenye vitabu au kuvikolezea wino kwenye tarakilishi<br>• atambue viambishi vya hali ya masharti katika hali kanushi (*k.v. singe, singali, sipo*)<br>• asome sentensi zenye viambishi lengwa kwenye vitabu au tarakilishi katika hali yakinishi na kanushi<br>• akanushe maneno na sentensi akizingatia hali ya masharti kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi<br>• kutunga sentensi sahihi zenye viambishi vya hali ya masharti na kuzikanusha<br>• asikilize au kutazama vipindi vya ukanushaji wa hali ya masharti kupitia vyombo vya kidijitali. | 1. Viambishi vya hali ya masharti katika vitenzi ni vipi?<br>2. Viambishi vya hali ya masharti katika ukanushaji ni vipi?<br>3. Unatumia viambishi gani wakati wa kukanusha vitenzi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika vikundi ili kujadili kuhusu ukanushaji.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapojaribu kukanusha maneno na sentensi.



Not for Sale

| | |
|---|---|
| • Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika somo. | |
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**:<br>• Stadi za Maisha – mwanafunzi anakuza uwezo wa kukubali au kukataa mambo mbalimbali maishani. | **Uhusiano na Maadili**:<br>• Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi za vikundi.<br>• Umoja – mwanafunzi anaposhiriki na wenazake katika kazi ya vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hushughulikia ukanushaji. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Mwanafunzi awe kielelelzo kwa wenzake na wanajamii katika kutumia Kiswahili ifaavyo katika mawasiliano. Aidha, awe makini kujifunza kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anatambua kwa usahihi viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anatambua viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anatambua baadhi ya viambishi vya hali ya masharti katika baadhi ya sentensi. |
| Kukanusha viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anakanusha kwa usahihi viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anakanusha viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anakanusha baadhi ya viambishi vya hali ya masharti katika sentensi. | Anakanusha baadhi ya viambishi vya hali ya masharti katika baadhi ya sentensi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.2 Ukubwa na Udogo wa Nomino:** Nomino zinazoanza kwa **Ki-**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ki-** katika kundi la maneno<br>b) kubadilisha nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo<br>c) kutunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>d) kufurahia kutumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** kwa usahihi katika hali ya ukubwa na udogo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi Ki- (*k.v. kiti, kitabu, kitanda*) kwa kutumia kadi za maneno, mti wa maneno, chati au vifaa vya kidijitali<br>• ashiriki kwenye mjadala wa kutambua viambishi vinavyotumika kudhihirisha ukubwa na udogo wa nomino<br>• ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo<br>• ashiriki katika mchezo wa vikundi ambapo kikundi kimoja kitataja wastani wa nomino na kingine kutaja ukubwa na udogo wa nomino hiyo<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino hizo katika hali ya | Je, ni nomino gani zinazoanza kwa kiambishi **Ki-** unazozijua? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ukubwa na udogo kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki mijadala kuhusu mada ya ukubwa na udogo wa nomino.
- Ubunifu – unadhihirika anapotunga sentensi sahihi katika hali ya ukubwa na udogo.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali wa wastani, ukubwa na udogo.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo mbalimbali katika shughuli za vikundi.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali katika mifano ya sentensi iliyotolewa kutegemea sentensi zilizotungwa. | • Heshima – wasikidharau kitu katika hali yake.<br>• Umoja – katika kufanya kazi kwenye vikundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – somo hili hushughulikia sarufi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwa kielelezo kwa kutumia lugha bora shuleni na katika huduma za kijamii huku akijifunza kutokana na matumizi ya lugha ya wanajamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **Ki-** katika kundi la maneno. | Anatambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ki-** kwa urahisi. | Anatambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ki-**. | Anatambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ki-**. | Anatatizika kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ki-**. |
| Kubadilisha nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. | Anabadilisha kwa wepesi nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. | Anabadilisha nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. | Anabadilisha baadhi ya nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. | Ana changamoto kubadilisha nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. |
| Kutunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga kwa urahisi sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ki-** katika hali ya ukubwa na udogo bila kuzingatia upatanisho wa kisarufi. |



Not for Sale

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.3 Ukubwa na Udogo wa Nomino:** **N**omino Zinazoanza kwa Kiambishi **Ji-**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** ili kuzibainisha<br>b) kubadilisha nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo<br>c) kutunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>d) kufurahia kutumia nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** kwa usahihi katika hali ya ukubwa na udogo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake kutaja nomino zinazoanza kwa kiambishi **ji-** katika hali ya ukubwa na udogo kwa kutumia kadi za maneno, mti wa maneno, chati au vifaa vya kidijitali k.v. jani (jijani - kijani), jiko (jijiko - kijijiko)<br>• ashiriki kwenye mjadala wa kutambua viambishi vinavyotumika kudhihirisha ukubwa na udogo wa nomino zinazoanza kwa kiambishi Ji-<br>• ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino hizo katika hali ya ukubwa na udogo kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. | Je, ni nomino gani zinazoanza kwa kiambishi **ji-** unazozijua? |

<table>
<tr><td colspan="2">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki mijadala kuhusu mada hii.<br>• Ubunifu – wanapotunga sentensi katika hali ya udogo.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali wa wastani na udogo.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Mshikamano wa kijamii – kutunga sentensi zinazolenga uraia mwema.</td><td>Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – wasividharau vitu katika hali yake.<br>• Umoja – katika kufanya kazi kwenye vikundi.</td></tr>
<tr><td>Uhusiano na Masomo Mengine<br>• Indigenous Languages – somo hili hushughulikia udogo wa nomino.</td><td>Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwa kielelezo kwa kutumia lugha bora shuleni na katika huduma za kijamii huku akiendelea kujifunza matumizi ya lugha kutokana na jamii.</td></tr>
</table>

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-**. | Anatambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** kwa urahisi. | Anatambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-**. | Anatambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-**. | Anatatizika kutambua nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-**. |
| Kubadilisha nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali wastani kuwa katika hali ya | Anabadilisha kwa wepesi nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali wastani | Anabadilisha nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali wastani kuwa katika hali ya | Anabadilisha baadhi ya nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali wastani kuwa katika hali ya | Ana changamoto kubadilisha nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali wastani |



Not for Sale

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ukubwa na udogo. | kuwa katika hali ya ukubwa na udogo | ukubwa na udogo. | ukubwa na udogo. | kuwa katika hali ya ukubwa na udogo. |
| Kutunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga kwa urahisi sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga sentensi sahihi akitumia nomino zinazoanza kwa kiambishi **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo huku akizingatia upatanisho wa kisarufi. | Anatunga baadhi ya sentensi akitumia nomino zinazoanza kwa **Ji-** katika hali ya ukubwa na udogo bila kuzingatia upatanisho wa kisarufi. |

**MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| Mada | Mapendekezo Ya Mbinu Za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| **1.0 KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye<br>e) orodha<br>f) Kuambatanisha maneno na majibu<br>g) Mijadala<br>h) Mazungumzo<br>i) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>j) Wanafunzi kufanyiana tathmini | ● Chati<br>● Michoro na picha<br>● Mgeni mwalikwa<br>● Vifaa vya kidijitali (k.v tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>● Mti wa maneno<br>● Kapu la maneno<br>● Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama mbalimbali shuleniVyama/vilabu mbalimbali shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **KUSOMA** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika | ● Tarakilishi/vipakatalishi<br>● Kinasasauti | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama mbalimbali shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kukariri na kuimba mashairi<br>e) Kusoma kwa sauti<br>f) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>g) Potfolio<br>h) Shajara | ● Rununu<br>● projekta<br>● Tarakilishi/vipakatalishi<br>● Kinasasauti<br>● Rununu<br>● projekta<br>● Nakala ya shairi<br>● Kamusi mbalimbali | mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **KUANDIKA** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | ● Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>● Kielelezo cha insha ya maelezo<br>● Kielelezo cha insha ya wasifu<br>● Nakala ya barua ya kirafiki<br>● Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama mbalimbali shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SARUFI** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kujaza fumbo maneno<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• projekta<br>• Kapu la maneno<br>• Mti wa maneno<br>• Kadi za maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro<br>• Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama mbalimbali shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |



Not for Sale